


**Rosa** Ree usitake kuwatoa udenda vidume

UKURASA 20



**Guardiola** amtaka Messi asiondoke Barca

UKURASA 21







UKURASA 9


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0580568

Jumapili Mei 2, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# NEEMA YAJA

• **Rais** Samia ahutubia Mei Mosi, aleta matumaini mapya... *Endelea Uk. 2 & 3*




## Wafanyakazi wataka kima cha chini 970,000/-

UKURASA 3

## Nyongeza mishahara yawekwa kiporo

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu


**MICHEZO** GOMES: TUPO TAYARI KWA KAIZER UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

## Wafanyakazi wanena

**Na Richard Makore,** MWANZA

BAADA ya serikali kutangaza kutoongeza mishahara katika mwaka ujao wa fedha, baadhi ya wafanyakazi wamesema wanalazimika kusubiri ahadi ya serikali kushughulikia suala hilo.

Katibu wa Chama cha Wafanyakazi wa Hifadhi, Majumbani na Hoteli (CHODAU) mkoani Mara, Malunde Majuna, alisema wataendelea kusubiri ahadi ya Rais Samia Suluhu Hassan ambaye amesema kuwa mwakani atangaza nyongeza ya mishahara.

Alisema licha ya kuwa hajapandisha mishahara, amepunguza kodi kwenye mishahara kwa asilimia moja na kuondoa riba ya asilimia sita kwa wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu.

Alisema kwa sasa wanufaika watakatwa asilimia 15 ya mishahara kwa ajili ya kulipia deni lao na kwamba hakuna tena kutozwa riba.

Katibu huyo alisema Rais Samia jana alianika mipango mingi ya nchi na kwamba anaamini suala la nyongeza ya mishahara atatekeleza.

Janety Paul, mwalimu aliyehudhuria sherehe za Mei Mosi jijini Mwanza jana, alisema kauli ya serikali imewavuruga kwa kuwa walikuwa na matarajio ya kuongezwa mishahara.

Alisema kwa muda mrefu mishahara yao haijapanda na kwamba kauli ya jana imezidi kuwaumiza kwa kuwa gharama za maisha zimepanda.

Hata hivyo, alisema wataendelea kusubiri mpaka itakapofika mwakani ili kuona kama ahadi ya serikali itatekelezwa kama alivyoahidi Rais Samia.

Elfrida Mkumbo kutoka Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU), alisema wataendelea kusubiri mpaka mwakani kama alivyoahidi Rais Samia.

Alisema bado wana imani na serikali na wataendelea kusubiri ahadi hiyo ambayo wanamini itatekelezwa kama ilivyoahidiwa.



Rais Samia Suluhu Hassan, akiagana na viongozi mbalimbali wa serikali na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), baada ya kulihutubia taifa, katika maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi), yaluiyofanyika jana kitaifa katika Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza. **PICHA: OMR**

# Samia aahidi neema wafanyakazi

**Na Richard Makore,** MWANZA

NI neema! Ndivyo unavyoweza kusema baada Rais Samia Suluhu Hassan, kuahidi mambo mazuri kwa wafanyakazi nchini.

Licha ya kuweka wazi kuwa hakutakuwa na nyongeza ya mshahara kwa watumishi wa umma hadi mwaka mwingine wa bajeti (2022/23), Mkuu wa Nchi huyo ameahidi kuchukua uamuzi katika mambo kadhaa ambayo yatakuwa neema kwa wafanyakazi.

Katika hotuba yake jana jijini Mwanza katika sherehe za maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani, Rais Samia alisema hakutakuwa na nyongeza ya mishahara kwa watumishi wa umma katika mwaka ujao wa fedha kutokana na hali ya uchumi kutokuwa nzuri.

Hata hivyo, aliahidi atatangaza nyongeza hiyo wakati wa Mei Mosi ya mwakani ana akazipa jukumu bodi za mishahara kufanyia kazi suala hilo.

Sherehe hizo ambazo zilizokuwa na kaulimbiu ya 'Maslahi Bora, Mishahara Juu, Kazi Iendelee', ziliingiwa simanzi baada ya kauli hiyo ya Rais kutolewa.

Alisema bodi hizo zitaanza kufanya kazi mara moja na kwamba zitakapomaliza, ikifika tarehe kama ya jana mwakani, atatangaza kuongeza mishahara.

Alikiri kwamba wafanyakazi wa serikali wanakabiliwa na tatizo la kutoongezwa mishahara kwa kipindi cha miaka sita mfululizo na suala hilo atalifanyia kazi.

"Kwa miaka sita watumishi wa umma hawajaongezewa mishahara yao na wale wa sekta binafsi mishahara yao haijaongezwa kwa miaka minane sasa," alisema.

Rais alisema mafanikio yoyote ya nchi yanatokana na nguvu za wafanyakazi na kwamba anatambua mchango wao katika kukuza uchumi. Katika kuhakikisha serikali inawatua mzigo wafanyakazi wakati wakisubiri nyongeza ya mishahara, Rais Samia aliahidi kupunguza makato na kodi kadhaa ikiwamo ya Lipa Kadri Unavyopata (PAYE).

Rais Samia pia alisema serikali itatumia mabilioni ya shilingi katika mwaka ujao wa fedha kulipa malimbikizo ya madai ya wafanyakazi na kuajiri watumishi wengine wapya wapato 40,000.

Alisema ajira mpya zitagharimu Sh. bilioni 239 na kwamba serikali imeendelea kulipa madeni ya watumishi mbalimbali wa umma.

Alisema tayari Sh. bilioni 74 zimetumika kuwalipa watumishi zaidi 36,000 wakiwamo walimu, zikiwa ni madeni mbalimbali.

Alisema madeni ambayo siyo ya mshahara yamelipwa kwa Sh. bilioni 18 na mengine yaliyobaki yanaendelea kulipwa.

Pia, akaahidi kupandisha vyeo watumishi takriban 91,000 katika mwaka ujao wa fedha huku akiagiza watumishi walioondolewa kazini kutokana na kuwa na elimu ya darasa la saba, walipwe stahidi zao. Vilevile, alitangaza kufuta ongezeko la asilimia sita kila mwaka katika deni la wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu inayotolewa na serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB).

Akizungumza kabla ya kumkaribisha Rais Samia, Katibu Mkuu Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA), Said Wamba, alisema kima cha chini cha mishahara kwa wafanyakazi nchini imeendelea kuwa duni huku gharama za maisha zikipanda.

***Soma habari zaidi ukurasa wa 3**

# TUCTA yataka kima cha chini 970,000/-

**Na Romana Mallya**

SHIRIKISHO la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) limependekeza kwa serikali kiwango cha mshahara cha kumwezesha mtu kuishi kianzie Sh. 970,000.

Akisoma mapendekezo ya shirikisho hilo jana mbele ya Rais Samia Suluhu Hassan katika maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani jijini Mwanza, Kaimu Katibu Mkuu wa TUCTA, Said Wamba, alisema wakati umefika wa kuwa na kiwango halisi cha kitaifa.

Wamba alisema utafiti wa TUCTA waliofanya mwaka 2006 kuhusu kima cha chini cha mshahara kinachomwezesha mfanyakazi kumudu mahitaji muhimu, ulibaini kwa wakati huo kilitosha lakini utafiti wa mwaka 2014 ulibaini kiwango kinachotosha ni Sh. 720,000.

Alisema licha ya kima hicho mpaka jana kutofikiwa, gharama za maisha zimeendelea kupanda na kuwaumiza wafanyakazi wa sekta zote wanaoishi chini ya mstari wa umaskini. "TUCTA inapendekeza kiwango cha kumwezesha mtu kuishi kiwe ni Sh. 970,000. Hata hivyo, wakati umefika wa kuwa na kiwango halisi kitaifa.

"Tunaomba serikali ipandishe mishahara kwa sekta zote za umma na binafsi mwaka huu," alipendekeza. Wamba alitaja jambo la pili katika mapendekezo yao kuwa ni serikali kushughulikia urasimu wa kujadili, kufunga na uidhinishaji wa mikataba ya hali bora kwenye sekta ya umma kupitia Msajili wa Hazina na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na kusababisha kushuka hamasa ya kazi.

Pendekezo lingine ni serikali kushusha kodi katika mishahara na marupurupu mengineyo ili kupunguza mzigo kwa wafanyakazi.

"Ucheleweshwaji mafao kwa wastaafu, tunaomba mifuko iwalipe wanufaika pamoja na riba kwa mujibu wa sheria, idadi kubwa hajalipwa na baadhi wamekaa takribani miaka mitatu, wapo waliofariki dunia kabla ya malipo na waliopo vitandani wanaugua," alisema.

Shirikisho hilo pia lilipendekeza uundwaji wa mabaraza ya wafanyakazi sehemu za kazi kwa maeneo ambayo hawajafanya hivyo na serikali isimamie.

"Serikali itoe mwongozo kwa taasisi zote kuhusu bima ya afya, baadhi hushindwa kutoa huduma hususani matibabu ya gharama kubwa. "Kuondolewa ndugu waliofikisha umri wa miaka 18 kwenye bima za afya ni tatizo kwa wafanyakazi kwa sababu umri huo bado ni tegemezi, serikali ione namna ya kutoa huduma kwao," Wamba aliwasilisha.

Pia, aliiomba serikali kulipa madeni sugu ya watumishi ikiwa ni pamoja na fedha za likizo, malimbikizo ya mishahara na upandishaji vyeo. Kadhalika, TUCTA iliitaka serikali itoe msimamo kwa waajiri ambao hawajatekeleza agizo la serikali kuhusu watumishi waliositishiwa ajira waliokuwa na kiwango cha elimu cha darasa la saba ambao waliajiriwa baada ya katazo la Mei 20, 2004 na mwaka 2017 waliondolewa na iliamriwa wapewe stahiki zao na mafao.

Pendekezo lingine ni serikali kufanya marekebisho ya sheria na tozo ya kuongeza thamani ya fedha ambayo ni asilimia sita kila mwaka inayotozwa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) kwa wanufaika wa mikopo pamoja na kuifanyia kazi tatizo la taarifa tofauti za deni la mnufaika zilizopo kwa mwajiri na kwenye bodi.

Kuhusu ajira kwa raia za kigeni, TUCTA iliiomba sheria izingatiwe na kuitaka serikali kuondoa urasimu wa vikwazo vya uwekezaji.

TUCTA pia iliishauri serikali kupitia Ofisi ya Kamishna wa Kazi kuhakikisha mawakala wa ajira wanaendelea na majukumu yao kwa mujibu wa sheria bila kujibadili kuwa waajiri. Akisoma salamu za waajiri, Mwenyekiti wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), Jayne Nyimbo-Taylor, alitaja matatizo wanayokumbana nayo kuwa ni mlundikano wa kodi ambao umekuwa chanzo cha kuongeza gharama ya kufanya biashara na kupunguza uzalishaji na ushindani.

HABARI KITAIFA

# Mwinyi ataja sababu ya mishahara kutopandishwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema serikali ina azma ya kutekeleza utaratibu wa kuimarisha viwango vya mishahara kwa wafanyakazi wa kada ya kati, uchumi utakapozidi kuimarika.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani yaliofanyika katika Ukumbi wa Sheikh Idrisa Abdul-Wakil Kikwajuni mjini Zanzibar.

Alisema wafanyakazi wa eneo hilo ni muhimu katika maendeleo ya taifa kwa vile ndilo lenye wataalamu, wakiwamo walimu, wafanyakazi wa afya na wengineo ambapo hivi sasa wanalipwa mishahara duni.

Alisema Serikali ya Zanzibar ina nia njema ya kuimarisha mishahara kwa wafanyakazi wa ngazi zote kwa awamu tatu, lakini ilishindwa kukamilika kutokana na kuibuka kwa ugonjwa wa corona na kuathiri ukusanyaji wa mapato.

Rais Mwinyi alisema serikali inalenga kuangalia upya utaratibu wa malipo ya kiinua mgongo kwa wafanyakazi waliostaafu, maarufu vikokotoo, ikiwa na lengo la kuwanufaisha, wakati huu ambao wafanyakazi na wastaafu wengi wanalalamikia utaratibu huo.

Akigusia upande wa wastaafu na wazee, Dk. Mwinyi alisema serikali itaendelea na juhudi za kuimarisha maslahi yao kwa kuhakikisha malipo ya viinua mgongo kwa wastaafu na pensheni jamii kwa wazee waliofikia umri wa miaka 70 zinaendelea kutolewa kwa wakati na bila usumbufu.

Alisema serikali inaangalia uwezekano wa kupunguza umri huo wa wazee pamoja na kuongeza kiwango cha posho pale hali ya uchumi itakapoimarika.

Rais Mwinyi, akizungumzia vikwazo mbalimbali vilivyoelezwa katika risala ya wafanyakazi, alisema serikali inavifahamu na tayari imeanza kuzichukulia hatua, hivyo akawataka wafanyakazi kuendelea kuvuta subira kwa imani ya kupatiwa ufumbuzi hatua kwa hatua.

Alieleza kuwa taratibu na tathmini za miundo ya utumishi serikalini inaendelea kushughulikiwa ili kuhakikisha watumishi wote wanapata haki zao pamoja na kujengewa mazingira bora ya kufanya kazi ili kuongeza ufanisi.

"Lazima tuendelee kujenga mazingira bora zaidi ya kuwafanya wananchi wajenge imani na wanufaike vizuri na huduma zinazotolewa serikalini pamoja na kuwaondolea urasimu na usumbufu usio na lazima," aliahidi.

Rais Mwinyi alitumia fursa hiyo kutoa shukrani kwa sekta binafsi kwa kushirikiana na serikali na kutumia fursa za uwekezaji ziliopo nchini.

Hata hivyo, alisema wadau hao muhimu kiuchumi wanapaswa kuzingatia sheria na wajibu wa kulipa kodi na tozo mbalimbali, kuwapa mikataba wafanyakazi pamoja na kuwawekea fedha zao katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF).

Aliwakumbusha wafanyakazi kutekeleza wajibu wao ipasavyo na kufanya kazi kwa bidii na nidhamu ili kufanikisha dhamira ya serikali ya kukuza uchumi na kuimarisha huduma za kijamii, akibainisha mafanikio ya serikali yanategemea mchango mkubwa kutoka kwao.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, alisema janga na corona liloikumba dunia, limeathiri ukuaji wa ajira Zanzibar, huku akiwashauri waajiri wote waliofunga ofisi zao kutokana na ugonjwa huo, kutafakari upya kwa kutambua wafanyakazi ni kiungo muhimu katika taifa.

Alisema wizara hiyo itaendelea kuimarisha ushirikiano na idara mbalimbali ili kuona sekta ya kazi inaimarika na kukuza ajira.

Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyaakzi Zanzibar (ZATUC) Mwalim Ali Mwalim, aliiomba serikali kuliangalia kwa makini suala la vikokotoo kwa msingi kuwa limekuwa likilalamikiwa na wafanyakazi na wastaafu wengi kutokana na athari zake.

Katibu Mkuu ZATUC, Mwatum Khamis Othman, alisema pamoja na mafanikio makubwa yaliofikiwa katika kuleta ustawi wa haki za wafanyakazi, alizitaja kero kadhaa zinazowakabili ikiwamo ukimya wa serikali katika kupandisha mishahara na viinua mgongo kwa wastaafu.

Mkurugenzi wa Jumuiya ya Vyama vya Waajiri Zanzibar (ZANEMA), Salah Salim Salah, aliwataka wafanyakazi kubadilika kwa kutoa huduma bora katika maeneo yao ya kazi kwa kuwa dunia sasa inakabiliwa na ushindani mkali.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akikabidhi zawadi ya mfanyakazi bora kwa Masoud Haji Juma kutoka Shirika la Bandari Zanzibar, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi), jijini Zanzibar jana. Kushoto ni Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla. **PICHA: IKULU**

## ... apunguza PAYE

**Na Richard Makore, MWANZA**

SERIKALI imepunguza asilimia moja ya Kodi ya Lipa Kadri Unavyopata (PAYE) katika mishahara ya wafanyakazi kutoka asilimia tisa ya sasa.

Rais Samia Suluhu Hassan, alitangaza uamuzi huo jana katika sherehe za Siku ya Wafanyakazi Duniani iliyofanyika kitaifa jijini Mwanza.

Alisema kodi hiyo inawaumiza wafanyakazi katika sekta mbalimbali nchini na kwamba unafuu huo wa asilimia moja utawasaidia kukabiliana na ugumu wa maisha wakati wakisubiri nyongeza ya mishahara atakayoitangaza katika sherehe hizo mwakani.

Alisema kila mfanyakazi anakatwa kodi hiyo na sasa anaishusha hadi kufikia asilimia nane.

Kuhusu mafao kwa wastaafu, Rais Rais Samia aliagiza mifuko ya hifadhi ya jamii kutowazungusha wastaafu ili mfanyakazi akimaliza utumishi wake alipwe haraka.

Aliagiza wastaafu wote wanaosubiri mafao yao waanze kulipwa haraka mpaka wamalizike na kwamba wahusika wasimamie suala hilo.

Kuhusu bima ya afya, Rais Samia alitangaza kuongeza umri wa wategemezi kuongezwa kutoka miaka 18 hadi 21 ambao wanastahili kupatiwa matibabu.

Akizungumza katika sherehe hizo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, alisema Siku ya Wafanyakazi ilianzishwa duniani mwaka 1860. Alisema lengo lake lilikuwa ni kudai maslahi bora ya wafanyakazi katika sekta mbalimbali na Shirika la Kazi Duniani (ILO) lilipendekeza siku hiyo iwe inaadhimishwa Mei Mosi kila mwaka.

# Samia afuta 'riba' mikopo ya HELSB

**Na Richard Makore,** MWANZA

SERIKALI imetangaza neema kwa wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu wanaoendelea kukatwa mikopo yao kila mwezi baada ya kufuta utaratibu wa deni kuongezeka kwa asilimia sita kila mwaka.

Mwongozo wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) unabainisha kwamba ili kulinda thamani ya fedha na kuufanya mfuko wa ukopeshaji kuwa endelevu, kutakuwa na ongezeko la asilimia sita kila mwaka katika mkopo wa kila mnufaika kuanzia tarehe ambayo alianza kupokea fedha.

Katika hotuba yake ya jana jijini Mwanza wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani, Rais Samia Suluhu Hassan, alisema kwa sasa makato ya asilimia 15 anayokatwa mnufaika yataendelea, lakini inafuta ongezeko la asilimia sita kila mwaka.

Alisema serikali imeamua kuchukua hatua hiyo ili kumpunguzia ugumu wa maisha mnufaika na kwamba kwa sasa hatakatwa hilo ongezeko la asilimia sita.

Mkuu wa Nchi huyo pia alipongeza HESLB kwa jitihada zake katika kukusanya fedha kutoka kwa wanufaika, akibainisha urejeshaji umeongezeka.

Makato yanayotajwa kuwa ya kinyonyaji katika urejeshaji wa mikopo ya elimu ya juu, yaliibua mjadala mkali bungeni hivi karibuni huku Spika wa Bunge, Job Ndugai, akiitaka serikali kuchukua hatua vinginevyo mikopo hiyo itageuka kuwa biashara ya kuumiza watoto wa maskini wanayoikimbilia.

Rais Samia pia aliagiza waliokuwa wafanyakazi wa kiwango cha elimu cha darasa la saba walipwe stahiki zao.

Alisema wafanyakazi hao ambao walikuwa waaminifu ambao walipata ajira kabla ya Mei 20, mwaka 2004 katika sehemu mbalimbali za nchi, wapewe haki zao.

Alikiri kwamba serikali iliwaondoa kazini na kwamba hakuna sababu ya kuwazungusha malipo kwa kuwa hiyo ni haki yao.

Rais Samia alibainisha kuwa katika kundi hilo, wafanyakazi 4,300 walirejeshwa kazini lakini wapo ambao hawajalipwa fedha zao na kwamba hakuna haja ya kuweka kisingizio serikali haijatoa mwongozo.

Alitaka waajiri popote nchini kutafuta fedha haraka na kuwalipa wafanyakazi hao ambao waliachishwa kazi.

"Kila mwenye haki alipwe haki yake kwa kuwa alifanya kazi katika kipindi alichokuwa mtumishi wa serikali," aliagiza.

Rais Samia pia alikumbusha maagizo yake kuhusu vibali vya kazi kwa raia wa kigeni na manyanyaso ya wafanyakazi mahali pa kazi, akiitaka wizara husika kushughulikia suala hilo.

Kuhusu kuunda mabaraza ya kazi, alisema taasisi 40 za serikali hazina chombo hicho na kuishauri sekta binafsi kuwa na utaratibu huo licha ya kwamba hakuna sheria inayoilazimisha kuwa nacho.

Aliwataka waajiri kuruhusu wafanyakazi kuanzisha vyama vya wafanyakazi huku akitaka taarifa za unyanyasaji katika sehemu za kazi zitolewe.

## 'Haya yanahitimisha utumishi wa mwalimu'

**Na Mwandishi Wetu**

TUME ya Utumishi wa Walimu (TSC), imebainisha mambo yanayoweza kusababisha mwalimu aliyeko katika Utumishi wa Umma kuhitimishiwa kazi yake.

Mkurugenzi Msaidizi wa Ajira na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC, Mectildis Kapinga, alibainisha mambo hayo alipowasilisha mada kuhusu majukumu ya tume katika masuala ya ajira na maendeleo ya walimu wakati wa mafunzo ya wajumbe wa kamati za wilaya zinazoshughulikia ajira na maadili ya walimu jijini Mwanza.

Kapinga alibainisha kuwa kwa mujibu wa Kanuni ya 9(1) (a) – (g) ya Kanuni za Utumishi wa Walimu za Mwaka 2016, mambo yanayoweza kumsababishia mwalimu ahitimishe kazi yake ya ualimu ni pamoja na kustaafu kwa kutimiza umri kwa mujibu wa sheria.

Alisema kuwa sababu nyingine ni kustaafu kwa ugonjwa, kuachishwa kazi kwa masuala ya kinidhamu, kufariki dunia, kuacha kazi kwa hiari, kustaafishwa kwa manufaa ya umma, kufutwa kwa ofisi na kugombea nafasi za uongozi hususan wa kisiasa.

Akielezea kuhusu utaratibu unaotumika wakati mwalimu anapohitimisha utumishi kwa kustaafu kwa lazima au hiari, Kapinga alisema ni pamoja na ofisi za TSC, ngazi ya wilaya kuandaa maoteo ya kustaafu kazi walimu kwa kila mwaka wa fedha na kuwasilisha nakala makao makuu ya tume na kwa mwajiri.

Vilevile, alisema utaratibu mwingine unaotakiwa kufanyika ni kwa mwalimu anayetarajia kustaafu kwa hiari au lazima, kutoa taarifa miezi sita kabla ya tarehe ya kustaafu kwake, ikiwa ni kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma.

Aliongeza kuwa Katibu wa Tume ngazi ya wilaya, anatakiwa kuandika kibali cha kustaafu kazi na kibali hicho kipitishwe na mwajiri kabla ya kukabidhiwa kwa mwalimu husika.

Katika hatua nyingine, Kapinga alisema kustaafu kwa lazima au kwa hiari kunategemea tarehe ya kuzaliwa kwa mwalimu, ambapo anaruhusiwa kustaafu kwa hiari afikishapo umri wa miaka 55 na atalazimika kustaafu kwa lazima afikishapo umri wa miaka 60.

Aliongeza kuwa, endapo itatokea kwenye kumbukumbu za kuzaliwa, mwalimu akawa alijaza mwaka bila tarehe, basi tarehe yake itakayotumika itakuwa Julai Mosi ya mwaka atakaostaafu.

"Ikitokea kuwa alijaza mwezi na mwaka bila tarehe, basi tarehe yake ya kuzaliwa itahesabika kuwa tarehe 15 au 16 ya mwezi huo," alifafanua.

Alisema kuwa endapo kutakuwa na mgongano wa tarehe ya kuzaliwa kwenye kumbukumbu za kiutumishi za mwalimu husika, tarehe itakayotambuliwa ni tarehe yake sahihi ya kuzaliwa ni ile inayompa umri mkubwa.

Mafunzo hayo yalihusisha wilaya zote za mikoa ya Kanda ya Ziwa na yalilenga kuwajengea uwezo wajumbe wa kamati husika ili watimize majukumu yao kwa ufanisi.



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, mkoani Songwe, Hanji Godigodi (kushoto), akitoka kwenye ukumbi wa mkutano juzi, baada ya Baraza la madiwani wa halmashauri hiyo, kupitisha azimio ka kutokufanya kazi naye kwa madai ya matumizi mabaya ya madaraka. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Madiwani wasusa kufanya kazi na DED

**Na Grace Mwakalinga,** MBOZI

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe, wameazimia kutofanya kazi na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Hanji Godigodi, kwa madai ya matumizi mabaya ya madaraka na kukwamisha katika shughuli za maendeleo.

Uamuzi huo uliafikiwa juzi kwenye kikao cha Baraza la Madiwani ambapo kwa pamoja walikubaliana kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo hafai kuongoza kutokana mwenendo wake kuwa mbaya.

Diwani wa Nyimbili, Tinson Nzunda, aliliambia baraza kuwa miongoni mwa tuhuma zinazomkabili mkurugenzi huyo ni matumizi mabaya fedha zinzotokana na makusanyo ya kahawa, ujenzi wa Stendi ya Vwawa, ujenzi wa Shule ya Msingi Kisimani, ukarabati wa magari ya halmashauri, kutolipa fedha kwa wazabuni na lugha chafu kwa watumishi na madiwani.

Nzunda alidai kuwa kwa kipindi kirefu mkurugenzi huyo amekuwa kikwazo kwao hali inayosababisha shughuli za maendeleo kukwama hivyo wameamua aondoke ili kupisha viongozi wengine watakaokuwa tayari kuwatumikia wananchi na kuleta maendeleo.

"Madiwani kwa umoja wetu tumeazimia kuanzia leo (juzi) hatumtaki mkurugenzi huyo, atupishe kwa sababu amekuwa kikwazo kwenye shughuli za maendeleo lakini pia hana lugha nzuri kwa watumishi wenzake, hata kwetu pia anatoa lugha za dharau, tunaomba aondoke tuletewa mkurugenzi mwingine," alisema Nzunda.

Diwani wa Halungu, Maarifa Mwashitete, ambaye ni mjumbe kwenye Kamati ya Fedha na Mipango, alidai kuwa mara kwa mara wamekuwa wakihoji matumizi ya fedha za miradi lakini walipohitaji ushirikiano kutoka kwa mkurugenzi, hakutimiza majukumu yake.

Alisema miongoni mwa maeneo waliyokuwa wanatilia shaka ni matumizi ya fedha zitokanazo na kahawa ambapo katika kikao kilichopita, walihoji makusanyo ya fedha zitokanazo na zao hilo kutoendana na uhalisia wa mavuno kwa wakulima.

Kutokana na hali hiyo, walihoji ukusanyaji wa mapato na kubaini ubadhirifu wa fedha ambapo walilazimisha Ofisa Ushirika kuchukuliwa hatua za kinidhamu ikiwamo kusimamishwa kazi baada ya kubaini wizi.

Alidai kuwa tuhuma nyingine ni gharama za matengenezo ya magari ya halmashauri ambapo walidai kiwango cha fedha kiilichoandikwa kwa ajili ya matengenezo kilikuwa kikubwa kuliko kilichotumika, hivyo wakaona mkurugenzi ana matumizi mabaya ya fedha.

Diwani wa Ihanda, Adam Mbuba, alidai mkurugenzi huyo hana ushirikiano mzuri na watumishi wenzake na hata madiwani kutokana na kauli mbaya anazozitoa ikiwamo kutoa lugha zisizofaa na dharau pindi wanapohitaji ufafanuzi.

Diwani wa Viti Maalum Tarafa ya Vwawa, Mesia Swela, alidai kuwa mkurugenzi amechangia kwa kiasi kikubwa kukwamisha shughuli za maendeleo hivyo hawataki kufanya kazi naye.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, George Msyani, aliungana na madiwani wenzake kuazimia kumwondoa mkurugenzi kwa madai hawako tayari kufanya kazi naye kutokana na mwenendo wa tabia zake.

Alisema kwa sasa, halmashauri hiyo ikaimishwe kwa Ofisa Mipango ambaye ataendelea na majukumu hadi pale watakapotafutiwa mkurugenzi

# Serikali yataka tathmini ya lishe

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imewataka maofisa lishe kwenye mikoa na wilaya nchini kukamilisha tathmini ya lishe kwenye maeneo yao ndani ya mwezi Julai mwaka huu, ili kutoa nafasi ya tathmini ya kitaifa itakayofanyika Agosti mwaka huu.

Agizo hilo lilitolewa jijini jana na Mkurugenzi wa Idara ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Dk. Ntuli Kapologwe, katika hotuba yake iliyosomwa na Mkurugenzi Msaidizi, Rasheed Maftaa, alipofunga mkutano wa mwaka wa maofisa hao.

Alisema utaratibu umewekwa wa kufanya tathmini ya mkataba wa lishe kitaifa kila mwaka. "Idara ina taarifa za uchambuzi wa mipango ya lishe kwa mikoa na halmashuari, ni jukumu lenu kuhakikisha kuwa changamoto zote zilizoonekana wakati wa zoezi zinafanyiwa marekebisho na kukamilisha mipango hiyo ifikapo Mei 30 mwaka huu," aliagiza.

Aliwataka maoafisa lishe kuhakikisha taarifa za lishe zinazojazwa katika Mfumo Jumuishi wa Tathmini na Ufuatiliaji wa Taarifa (IMES), zinajazwa kwa usahihi, kuhakikiwa na kutumwa Makao Makuu TAMISEMI kwa wakati.

"Ninatambua kwa sasa tunao mfumo wa IMES, uwapo wa mfumo huu uwe ni nyenzo muhimu ya kutuwezesha kuwa na takwimu sahihi ambazo zitatusaidia katika mipango yetu," alisema.

Alisisitiza agizo la Katibu Mkuu TAMISEMI, Prof. Riziki Shemdoe, alilolitoa wakati wa ufunguzi, kwa kuitaka mikoa ikarejee miongozo ya utoaji wa Sh. 1,000 inayotengwa kwa kila mtoto aliye chini umri wa miaka mitano inazingatiwa kwa kutengwa kama mwongozo unavyoelekeza.

HABARI KITAIFA

# TFS yawabana waliopewa miti

Na Mwandishi Wetu

SERIKALI imewataka wafanyabiashara wanaovuna miti katika Shamba la Miti Shume, kuhakikisha wanalipia na kuvuna mita za ujazo walizopewa kwa mwaka huu wa fedha kabla mgao haujafanyika kwa wengine.

Akizungumza katika mkutano wa wafanyabishara hao uliondaliwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Naibu Kamishna wa Uhifadhi TFS, Mohamed Kilongo, alisema ikiwa imebaki miezi miwili mwaka wa fedha kuisha, serikali imeona ni vyema ikakutana na wafanyabiashara na wananchi inayowahudumia kuzibaini kero zao na kutafuta namna ya kuzitatua ili kuongeza kasi ya uvunaji.

"Tumekuja hapa kuwasikiliza ni nini ambacho tunatakiwa kukiongeza zaidi ili tuweze kuvuna kwa kasi.

"Hadi sasa uvunaji uko asilimia 48 huku ikiwa tumebakiza miezi miwili tu tufunge zoezi la uvunaji katika mwaka huu wa fedha, uvunaji uko chini na una athari kubwa kwa pande zote mbili za wafanyabiashara na serikali," alionya.

Naibu Kamishna huyo alisema wafanyabiashara licha ya kupewa mgao huo, hawajafanya biashara huku upande wa pili (serikali) ukishindwa kufikia lengo la makusanyo na hivyo kukwamisha miradi ya maendeleo na matumizi mengine ya serikali kwa sababu ya wafanyabiashara hao kushindwa kulipa na kuvuna miti waliyoomba kuvuna.

Alisema anajua kwa sasa soko la mbao limekuwa gumu kwa wavunaji wa mashamba ya miti ya serikali kutokana na soko la mbao changa kushika kasi kwenye soko la ndani huku lile la nje likikwamishwa na Covid-19. Alisema kuwa pamoja na kikwazo hicho, wapo wafanyabiashara waliomaliza kuvuna maeneo waliyoomba lakini wanashindwa kupewa mgao mwingine kutokana na wengine kuendelea kushikilia mgao wao licha ya kushindwa kuvuna, na hivyo kumwagiza Mhifadhi wa Shamba la Miti Shume kuhakikisha anawabana wale wote walioshindwa na kuwapa wale wenye uhitaji. Mhifadhi wa Shamba la Miti Shume, Ernest Madata, alisema kwa kutambua kuwa msimu wa uvunaji unaelekea ukingoni, alifanya kikao na wavunaji hao wiki iliyopita na kukubaliana ifikapo Jumatatu Mei 3 mwaka huu, yaani kesho, wafike ofisini na kusema katika kipindi cha mwezi mmoja uliobaki kiasi gani wanaweza kuvuna ili taratibu zingine zifanyike.

"Kwa sababu tunaelekea ukingoni mwa msimu wa uvunaji wa mwaka wa fedha 2020/21 na kuna wateja ambao wako chini sana, tulikaa kikao na kukubaliana kwamba Jumatatu waje waseme katika migao yao ni kiasi gani wanaweza kuliupia na kuvuna katika kipindi cha mwezi mmoja uliobaki ili kiasi kinachobaki kiweze kutolewa kwa wavunaji wenye uhitaji kuliko kuendelea kuikosesha serikali mapato," alisema.

Ally Masoud, mmoja wa wafanyabiashara wanaovuna katika shamba hilo aliyemaliza mgao wake, alisema anashukuru kwa uamuzi huo utakaomwezesha kukamilisha uvunaji wake na kuwataka wafanyabishara wenzake kushirikiana katika kuonyeshana fursa za masoko.



Mwendesha pikipiki akipita jirani na nguzo ya umeme inayokaribia kuanguka kwa takribani wiki moja sasa na kuhatarisha usalama wa watumiaji wa barabara ya eneo la nyumba za viongozi, Mikocheni, mkoani Dar es Salaam jana. PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE

# Vijana balehe wapewa somo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIBU Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii), Dk. John Jingu, amewataka wasichana balehe kulinda ndoto zao na kujiepusha na vishawishi vitakavyoharibu ramani ya maisha yao.

Dk. Jingu alitoa rai hiyo jana jijini hapa alipofunga mkutano wa mwaka wa wadau wanaotekeleza Afua za Maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI (VVU) na UKIMWI zinazolenga wasichana balehe na wanawake vijana.

Alisema endapo wakijitambua, hawatakuwa tayari kurubuniwa na itakuwa rahisi kwao kukataa vishawishi.

"Hakikisheni mnasema hapana na maana ya kusema hapana ni kuepuka marafiki wabaya na wenye ushawishi mbovu, vitu vizuri huwa vinachukua muda, msiwe na papara na kikubwa mlinde ndoto zenu msizipoteze.

"Ninaomba wasichana mjitambue na kujiamini kwani ni nyenzo muhimu ya kutatua changamoto zinazoendana na umri wenu.

"Jiamini unaweza kupambana na changamoto, Ukilegea kidogo, ukiteleza unaharibu ramani ya maisha yako," alionya. Alisema kujiamini kwa vijana balehe na kujitambua kwao ni nyezo muhimu ya kupambana na vikwazo vya maisha ikiwamo VVU.

Katibu Mkuu huyo alivitaka vyuo na shule nchini kuanzisha madawati ya jinsia ili vijana wanaopata vikwazo na kufanyiwa vitendo vya ukatili, wapate msaada. Alisisitiza umuhimu wa nguzo kuu sita za ajenda ya kitaifa ya kuwekeza katika afya na maendeleo kwa vijana balehe ambazo ni kuzuia maambukizi VVU kwa vijana, kutokomeza mimba katika umri mdogo, kuzuia ukatili wa kimwili na kisaikolojia na kuboresha lishe miongoni mwa vijana balehe.

Alitaja nyingine kuwa ni kuhakikisha watoto wanapelekwa shule na kumaliza masomo yao na kuwawezesha vijana balehe kupata fursa za kiuchumi kwa kuajiriwa na kujiajiri.

Alihimiza mashirika yasiyo ya kiserikali na taasisi mbalimbali kuendelee kulilinda na kulisaidia kundi hilo.

Mkurugenzi Mkuu Tume ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS), Dk. Leonard Maboko, alisema nia ya serikali kufikisha afua za mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI kwa kuwezesha vijana kupata fursa za mitaji na ajira, ni kuondokana na vishawishi wanavyokumbana navyo. Mmoja wa wawakilishi wa wasichana balehe na wanawake vijana, Mariana Mathias, kutoka mkoani Mbeya, alishukuru serikali na wadau kuja na afua mbalimbali zinazolenga kuwasaidia ambazo zimesaidia kujiamini na kujitambua.

# Serikali yatambua uhuhimu wa wadau wa mazingira

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI imesema itaendelea kutambua mchango wa wadau na taasisi mbalimbali zinazojitoa katika utuzaji wa mazingira nchini na itawaunga mkono katika kila hatua na mapendekezo watakayoyatoa ili kuhakikisha taifa linakuwa na mazingira salama.

Kauli hiyo ilitolewa Dar es Salaam jana na Mkurugenzi wa Idara ya Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais, Endrew Komba, alipozungumzia mchango wa taasisi hizo likiwamo Shirika la Kimataifa la Uhifadhi wa Mazingira na Wanyama Pori (WWF).

Alisema taasisi hizo zimekuwa zikishirikiana na serikali kwa muda mrefu katika maeneo yote ambayo serikali imekuwa ikiyafanyia kazi ikiwamo uhifadhi, masuala ya asili na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi ili kupunguza madhara na kuleta ustahimilivu wa jamii katika masuala ya mazingira.

"Sisi kama serikali tunazichukulia taasisi hizi kama wadau wakubwa sana ambao wanatusaidia sisi katika kuhakikisha jamii yetu inaishi katika mazingira ambayo ni endelevu, hivyo tutashirikiana nao katika suala la utunzaji wa mazingira nchini," aliahidi.

Komba alisema serikali itatoa mchango wa kisera, miongozo na kuweka vipaumbele stahiki ambavyo vitawezesha wadau wa mazingira kufanya kazi kwa urahisi nchini.

Alisema taasisi hizo zinasaidia pia katika kuleta mawazo ya maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani na zimekuwa zikitoa mchango wa kifedha ili kuhakikisha kuwa siku hiyo inaadhimishwa vizuri na mwaka huu itafanyika Juni 6 jijini Dodoma, ikiwa na dhumuni la kukumbusha na kusisitiza umuhimu wa utuzaji wa mazingira kwa maendeleo ya taifa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wafanyakazi wanapaswa kuwa na uvumilivu kuhusu nyongeza za mishahara

**WAFANYAKAZI** nchini, jana waliungana na wenzao duniani kote kusherehekea Siku ya Wafanyakazi, marufu kama Mei Mosi. Kitaifa, maadhimisho hayo yalifanyika katika Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza.

Licha ya kufanyika kitaifa katika jiji hilo na Rais Samia Suluhu Hassan kuwa mgeni rasmi, maadhimisho hayo pia yalifanyika sehemu mbalimbali nchini kwa wafanyakazi kufanya maandamano na viongozi wa mikoa kutoa hotuba zao.

Visiwani Zanzibar, Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alikuwa mfgeni rasmi katika maadhimisho yaliyofanyika kwenye ukumbi wa Sheikh Idris Abdulwakil, Kikwajuni, Zanzibar.

Kutokana na kiu ya muda mrefu ya wafanyakazi kupata nyongeza za mishahara, matumaini yao makubwa yalikuwa hayo kwamba Rais Samia angetangaza neema juu ya matamanio hayo.

Hata hivyo, Rais Samia hakufanya hivyo na badala yake akaahidi kulifikiria suala hilo katika bajeti ya mwaka 2022/23. Wakati Rais Samia akiahidi hivyo, Dk. Mwiyi aliweka bayana kwamba nyongeza za mishahara zitatolewa baada ya hali ya uchumi kuimarika.

Kwa mantiki hiyo, wafanyakazi wanatakiwa kuwa wavumilivu hadi muda ulioahidiwa utakapowadia na wakati huo huo wanapaswa kuchapa kazi kwa ari na bidii ili kuleta tija na ufanisi, ambavyo vichocheo katika ukuaji wa uchumi na pato la mtu mmoja na taifa kwa ujumla.

Sababu zilizoelezwa na Rais Samia na mwenzake kwa upande wa Zanzibar, zinatosha kuonyesha uhalisia wa jambo lililokuwa likitarajiwa na wafanyakazi. Sababu hizo ni hali halisi ya sasa ya uchumi ambayo iliathiriwa kwa kiasi kikubwa na janga la corona ambalo bado linaisumbua dunia.

Kama wahenga wasemavyo subira yavuta heri, wafanyakazi wanapaswa kuwa wavumilivu huku wakiomba hali yua uchumi itengemae na wakati huo huo wakiendelea kuchapa kazi na kushiriki kwa namna mbalimbali kukuza uchumi wa nchi.

Pamoja na kuwa na subira, wafanyakazi wametangaziwa neema kutokana na kupunguzwa kwa kodi itokanayo no mishahara, maarufu kama PAYE, kwa asilimia moja. Kupunguzwa kwa kiwango hicho kutaleta unafuu katika vipato vya wafanyakazi na hatimaye kuwa na ahueni kimaisha.


Licha ya kupunguzwa kwa kodi hiyo, watumishi wa umma kumeibuka neema zaidi kwa kuwa kati ya watumishi 85,000 na 91,000 watapandishwa vyeo na madaraja. Kwa maana hiyo, kutakuwa na nyongeza zisizo za moja kwa moja za mishahara. Kupandishwa vyeo na madaraja kunamaliza kilio cha miaka mingi cha watumishi wa umma kutokupata fursa hiyo.

Kwa jumla, hotuba ya Rais Samia pamoja na ile ya Dk. Mwinyi, zimeleta matumaini makubwa kwa wafanyakazi wa umma na sekta binafsi kwamba baadhi ya matatizo yao yanayohusu maslahi yameanza kupatiwa ufumbuzi.

Nyota njema huonekana asubuhi, ndivyo wahenga wasemavyo. Viongozi hao ambao wamehutubia kilele cha Siku ya Wafanyakazi nchini tangu waliposhika hatamu za uongozi, wameonyesha njia kwamba hatua kwa hatua maslahi ya wafanyakazi yanaanza kupatiwa ufumbuzi.

Jambo la msingi kwa wafanyakazi ni kuvuta subira kwa sababu kila jambo hufanywa kwa hatua, hivyo kuna matumaini kwamba wakati utafika na kilio chao kitasikilizwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Kero hizi nje ya stendi ya Mbezi zitafutiwe ufumbuzi

**"MAJI** lita moja na nusu Sh. 500, kule ndani ni Sh. 1,000, karibuni huku".

Ni maneno ya mmoja wa wafanyabiashara wadogo walioko nje ya stendi ya mabasi ya mikoani iliyoko Mbezi Luis, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam.

Anatamka maneno hayo akiita wateja ambao wengi wao ni abiria wanaofika katika stendi hiyo kutafuta usafiri wa kwenda mikoa mbalimbali na wakiwamo pia wanaosafiri kwenda nchi jirani.

Stendi hiyo inayotajwa kuwa ya kisasa, ilifunguliwa rasmi Februari, mwaka huu, na aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dk. John Magufuli, na kufungwa kwa ile ya zamani iliokuwa Ubungo.

Tangu kufunguliwa rasmi na kuanza kutoa huduma, tayari wamachinga wamejazana mbele ya stendi hiyo, wakiwa wameweka miavuli, vibanda na meza za biashara mbalimbali zikiwamo za maji ya kunywa.

Kuwapo kwa wamachinga hao mbele ya stendi hiyo, kunaweza kuhatarisha baadhi ya biashara ya wale ambao wamekodisha fremu zilizomo ndani ya stendi hiyo iwapo mamlaka husika hazitaliona tatizo hilo.

Kwa mfano, mfanyabiashara amekodisha fremu ya kuuza maji ndani ya stendi, halafu nje kuna mwingine anauza maji kama hayo na tena kwa bei nafuu, kweli yule wa ndani anaweza kupata wateja?

Mmachinga yuko nje anauza maji ya lita moja na nusu kwa Sh. 500 lakini mfanyabiashara ambaye yuko ndani ya stendi anauza maji hayo kwa Sh. 1,000, ni wazi kwamba mteja atanunua nje.

Iwapo hali itakuwa hivyo, ni wazi kwamba mfanyabiashara wa ndani ataendelea kukosa wateja na mwisho anaweza kujikuta amekwama kulipa kodi na hivyo kulazimika kufunga biashara.

Nimetaja muuza maji kwani nilisikia akitangaza bei, huku akiwaambia wateja wasiende kununua ndani kwa madai kwamba yanauzwa kwa bei iko juu. Kama itakuwa hivyo katika biashara nyingine, maana yake kuna tatizo.

Hali hiyo inaweza kuchangia kuikosesha mamlaka ya serikali ya mtaa ya eneo hilo mapato kama ambavyo ilielekeza wafanyabiashara kujaza fomu kwa ajili kukodi fremu za biashara ndani ya stendi hiyo.

Kwa kuwa ilielezwa kwamba pembezoni mwa stendi hiyo yenye sehemu ya juu na chini kumejengwa eneo maalumu kwa ajili ya wamachinga na mama na baba lishe, basi ingependeza wakipengwa sehemu husika.

Utaratibu uliokuwa umetangazwa na jiji (wakati huo) ni kwamba wamachinga, mama na baba lishe walitakiwa kuandika barua ya kuomba kufanya biashara kwenye maeneo waliotengewa na kuwasilisha utambulisho kutoka kwa Mtendaji wa Serikali ya mtaa anapoishi mwombaji.

Kwa jinsi hali ilivyo nje, inawezekana hawajafuata utaratibu huo, badala yake wakaamua kuchukua biashara zao na kuzipanga kando ya barabara inayoingia katika stendi hiyo.

Iwapo kinachoendelea nje ya stendi hiyo ndivyo kilivyo, basi ni vyema mamlaka husika zikifanya kila liwezekanalo kusaidia watu hao kuwaweka maeneo rasmi ambayo ni fremu walizotengewa kwa ajili ya kukodisha.

Lakini pia hatua hiyo itasaidia kumaliza kero zinazotokana na msongamano wa wamachinga waliojazana nje ya stendi hiyo, hali ambayo inaweza kusababisha hata wakati mwingine abiria kuibiwa.

Wingi wao huo wakati mwingine ni hatari kwa usalama wao, kutokana na kwamba wanapanga biashara kando ya barabara inayoingia stendi, na ikitokea gari likamshinda dereva, linaweza kuwagonga.

Kwa kuwa wamachinga, mama na baba lishe nao wanachangia kulipa kodi, ni vyema wakaboreshewa mazingira, ili kuepuka mtindo huo wa kupanga biashara kando ya barabara wakati fremu za kukodisha zipo.

Wakati wakiendelea na biashara katika eneo hilo, wingi wao pia unachagizwa na uwepo wa wapigadebe ambao awali kabla ya kufunguliwa kwa stendi, uongozi wa jiji ulitangaza kuwa hataruhusiwa kuonekana hapo.

Kinyume chake, wapigadebe wamezagaa huku wakiendelea kusababisha usumbufu kwa abiria, ikiwamo kuvuta kila mmoja akitaka kumwelekeza katika ofisi za mabasi ambayo wahusika wake wanampa chochote.

SAFU

AFYA

# Stafeli habari kubwa kwa afya ya binadamu

Na mwandishi Wetu

STAFELI ni tunda maarufu ambalo linaweza kuliwa kama tunda au kutengenezwa sharubati (jiusi). Kwa jina linguine, hujulikana kama topetope. Haijulikani kwa nini linaitwa hivyo lakini huenda ni kutokana na umbile lake hasa likiwa limeiva kwani huwa laini mfano wa tope.

Ni tunda linaloelezwa kuwa na faida nyingi ikiwamo uponyaji wa magonjwa mbalimbali. Unywaji wa maji yatokanayo na majani, mizizi au magamba yake, unaweza kunywa kama chai au kinywaji kingine cha kawaida.

Stafeli lina virutubisho vingi vikiwamo Amino Acid, Acetogeninc, Vitamin C, madini chuma, kalsiamu na Niacin, kutokana na virutubisho hivyo na vingine vingi, stafeli linaelezwa kuwa na faida nyingi kwa afya ya binadamu.

**Kupambana na saratani**

Ingawa si tiba ya moja kwa moja kwa saratani, tunda hili linaelezwa kuwa na virutubisho vyenye uwezo wa kupambana au kupunguza makali ya saratani.

Ukweli uliogundulika kutokna na utafiti wea masuala ya tiba na lishe unabainisha kuwa wagonjwa wa saratani wamepata njia nyingine mbadala ambayo haikuwapo awali.

Kwani hivi sasa wanaweza kulitumia stafeli kama dawa ya kupunguza makali au kuwapa kinga dhidi ya saratani. Pia wanaweza kuitumia pamoja na matibabu wanayopewa ya mionzi na kupata ahueni kubwa.

Takribani majaribio 15 ya kimaabara yaliyofanywa kuhusu uwezo wa stafeli, yamebaini yafuatayo:

●Huua chembechembe za saratani (cancerous cells) aina 12, ikiwamo saratani ya matiti, mapafu, kongosho, kibofu na tumbo.

●Stafeli lina mchanganyiko wenye uwezo mkubwa wa kudhibiti ukuaji wa seli za saratani mara 10,000 zaidi ya dawa ya 'Adriamycin' ambayo ndiyo hutumika kutibu aina mbalimbali ya saratani.

●Mchanganyiko wa virutubisho vya 'Annonaceous' 'Acetogenins' vilivyomo kwenye stafeli, huuwa seli zilizoathirika tu na saratani, tofauti na dawa za kisasa ambazo zenyewe huua seli zilizoathirika na hata zisizoathirika.

●Stafeli hudhibiti ukuaji wa seli za saratani bila kusababisha madhara mengine kama ilivyo kwa dawa za kisasa ambazo mgonjwa anapozitumia, iwe zile za njia ya mionzi, sindano au vidonge, huwa zina athari mbaya kwa mtumiaji na wakati mwingine humsababishia matatizo mengine ya kiafya.

**Kipanda uso**

Miongoni mwa virutubisho vilivyomo katika tunda hili ni pamoja na 'riboflavin' ambavyo husadia kutoa nafuu kwa ugonjwa wa kichwa cha kipanda uso.

**Upungufu wa Damu**

Kutokana na kuwa na wingi wa madini ya chuma, stafeli inasaidia kwa kiasi kikubwa kupambana na tatizo la kukauka au kupungua kwa damu mwilimi , maarufu kama 'Anaemia'.

**Tiba Magonjwa ya Ini**

Hii ni habari njema kwa watu wanaosumbuliwa na magonjwa ya ini. Licha ya tunda lenyewe kuwa tiba tosha kwa maradhi mbalimbali, juisi yake ina uwezo mkubwa katika matatizo ya kwenye ini na uvimbe kwenye kibofu cha mkojo.

**Kuimarisha Mifupa**

Stafeli ni chanzo kizuri pia cha madini ya shaba (copper) na kalshiamu, virutubisho ambavyo huwa muhimu kwa ukuaji wa mifupa mwilini.

Matatizo mengine yanayoweza kudhibitiwa na stafeli ni pamoja na kuumwa miguu, maumivu kwenye vifundo vya mikono na miguu, mwili kukosa nguvu na matatizo mengine ya viungo.

Licha ya faida hizo, stafeli pia lina umuhimu mkubwa kwa afya ya binadamu kutokana na kusaidia;-

● Kutibu maumivu ya nyuma ya mgongo (low back pain).

●Kutibu maumivu ya jongo (gout). Hili ni tatizo ambalo linawakumba watu wengi


● Kurekebisha usawa wa kiasi cha damu na sukari mwilini.

●Kuongeza kinga ya mwilini

● Kudhibiti ukuaji wa bakteria, virusi, vijidudu nyemelezi na uvimbe.

●Kuongeza stamina ya mwili na kurahisisha kupona haraka unapokuwa mgonjwa.

● Kutibu jipu na uvimbe.



**Majani, Mizizi pia Dawa**

Mbali ya tunda lenyewe kuwa na faida nyingi kama zilivyoanishwa hapo juu, vilivyomo vingine kwenye mti huo kama vile mizizi, majani, mbegu na magamba yake ni dawa ya magonjwa mbalimbali.

Inaelezwa kwamba unywaji wa maji yaliyotengenezwa kutokana na majani ya mstafeli hutibu magonjwa ya ngozi, chunusi na uvimbe wa mwili.

Aidha, maji ya majani ya mstafeli hutibu ugonjwa wa kuhara, kukohoa, kuvimba miguu, mapunye kichwani. Pia maji ya majani ya mstafeli yamethibitika kushusha kiwango cha sukari mwilini. Mbegu zake hutengenezwa dawa ya kula na kufukuza wadudu waharibifu.

Majani ya mti wa mstafeli hutumika kutibu maumivu ya mishipa. Saga majani yake mpaka yalainike kabisa, kasha paka taratibu eneo la mishipa lililo na maumivu mara mbili kwa siku.

**TAHADHARI**

Inaelezwa kwamba stafeli linaweza kuwa si salama kwa wajawazito, wagonjwa wa presha ya kupanda au kushuka, hivyo wanashauriwa kabla ya kula, wapate ushauri wa daktari. Lakini pia stafeli kwa asili yake lina kiasi kingi cha virutubisho vinavyoua bakteria, hivyo ulaji wa muda mrefu wa tunda hili unaweza kuua bakteria wote tumboni hata wale wazuri.

Kutokana na hali hiyo, iwapo mtu atakula tunda hili kwa zaidi siku 30 mfululizo, anashauriwa kuongezea na dawa za kulainisha njia ya chakula.

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Tuwe na Rais Samia si Mama Samia



Na Joseph Kulangwa

**Mawe kwa Kihaya ni mama yangu. Sasa kwa umri wa Mzee Kahama, kulia mama yangu ina maana kubwa, kwamba kwa kweli mama ni mama na mama ni kila kitu katika maisha ya binadamu. Hutasikia baba yangu au baba wee au tateee!**

MTOTO anapoanza kujifunza kutamka maneno, mara nyingi neno 'mama' humjia haraka na kirahisi, na kila apatapo shida, huita mama. Hata siku moja hutamsikia kuita baba.

Anamwona mama kuwa ni kila kitu maishani mwake, na ndiye anayeweza kumsaidia kutatua kila tatizo alilonalo, hata kama hajui tatizo ni nini, pengine hiyo inatokana tu na jinsi ya maumbile na uumbaji wa Mungu.

Haishangazi pia, kusikia jitu zima au zee zima, linapopatwa na matatizo, kuita mama. Si mara moja au mbili, mtu mzima akipatwa na ajali mathalan, utasikia analia "mama weee!"Haishangazi mtu kushitukia jambo ukamsikia akiita "mama yangu!"

Nakumbuka siku moja mwaka 1995 pale hoteli ya Kilimanjaro, Dar es Salaam, Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere akizungumza na wanahabari, alichomekea utani kuhusu mtani wake, Sir George Kahama aliyepata kuwa mmoja wa mawaziri wa kwanza katika Serikali yake.

Mwalimu alisema: "Siku moja nikamtuma Sir George kwenda Congo. Alipanda ndege, basi ndege ile ikakumbana na dhoruba angeni, iliporuka juu akasema 'my God', ikaruka tena akasema 'Mungu Wangu' safari ya tatu ikaruka juu zaidi, akasema 'maweeee'!

Mawe kwa Kihaya ni mama yangu. Sasa kwa umri wa Mzee Kahama, kulia mama yangu ina maana kubwa, kwamba kwa kweli mama ni mama na mama ni kila kitu katika maisha ya binadamu. Hutasikia baba yangu au baba wee au tateee!

Lakini hata katika kutukana, utasikia watu wanatukanana kwa kutumia majina ya mama, wakiamini kwamba mtu ukimtukania mama yake ndipo utakuwa umempata na umemuumiza. Watu hawajali kuwatukania baba zao, hata siku moja. Hapana haja ya kujiuliza, ila ndivyo ilivyo.

Inabaki kuwa ukweli tu, kuwa mama ni roho ya familia na bila mama familia inayumba. Mtu akimwona mama yake yupo, hata kama mtu huyo ni mzee kiasi gani, hupata faraja ya moyo na kujiona yuko salama.

Watanzania hivi sasa tumempata mama. Tuna kiongozi mmama. Tuna Rais wa Jamhuri mmama au mwanamke. Ndiyo sababu watu wanamwita Mama Samia Suluhu Hassan. Wakifupisha, utawasikia wakisema Mama kasema, au Mama Samia kasema. Mama Samia kanguruma, nakadhalika.

Utawasikia watu katika kona mbalimbali, wakitamba, kuwa Tanzania sasa imepona kwa sababu imepata mama. Utasikia kuwa hotuba za Mama zinatia faraja. Tanzania imerejeshewa furaha, kutokana na hotuba za Mama.

Wapo wengine wanaosema Mama Samia ni sawa na muuguzi, anakuchoma sindano huku akikwambia pole. Mama Samia anang'ata na kupuliza, hivyo hupati maumivu hata kama anakupiga dongo! Wanasenma Mama Samia hafoki, lakini anakupa makavu.

Mama Samia, kama watu wanavyomwita sana, amekuwa muwazi na anataka Tanzania isonge mbele, anataka ya nyuma yasiyo mema yaachwe na tugange mema yajayo, anataka kuonana na kila kundi nchini, ili kujua linafikiria nini, na nini kifanyike nchi isonge mbele.

Kaingia na mguu mzuri, kapokewa na mkono mzuri na wananchi. Bila shaka kazi iliyoanzishwa na hapa kazi tu itaendelea, lakini pengine kwa mtindo tofauti na wa Hapa Kazi Tu, ili mradi ikiwa na lengo zuri la kumsaidia Mtanzania.

Lakini pamoja na kwamba tunatambua ni mama au kama apendavyo kusema yeye ni Rais katika maumbile ya mwanamke, bado anastahili kutambulishwa kama Rais Samia Suluhu Hassan na si marazote kumtambulisha kama Mama Samia, kwa sababu huko nyuma hatukupata kuwatambulisha viongozi wetu hivyo.

Sikumbuki kumtambulisha Baba Julius Kambarage Nyerere, Baba Ali Hassan Mwinyi, Baba Benjamin William Mkapa, Baba Jakaya Mrisho Kikwete au Baba John Pombe Magufuli, ila Rais fulani, fulani, fulani, fulani, fulani.

Ili kumtofautisha na kina mama wengine, tuache kumwita mama au wengine wakimwita Bi Mkubwa, bali tujikite katika kumtambulisha kwa wadhifa wake na kumpa heshima stahiki, miongoni mwa marais wenzake Afrika na duniani. Alamsiki!

## KONA YA UKWELI



Na Thobias Mwanakatwe

**Lakini ni jambo lililo wazi kuwa tangu Bunge la 12 limeanza vikao vyake, tumeshuhudia wabunge hususani wa kutoka chama tawala wakitoa hoja nzito za msingi na wakati mwingine kuibana serikali ili ifanye yale ambayo wananchi wanayataka.**

# *Katika hili Makamba umesema kweli*

SIKU moja nikiwa katika majukumu ya kazi zangu zinazonipatia riziki, nikapata wasaa wa kufuatia vikao vya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania vinavyoendelea hivi sasa jijini Dodoma, kupitia redio.

Kimsingi, mimi ni mmoja watu wanaopenda kufuatilia sana Bunge ili kujifunza mengi kutoka kwa waheshimiwa wabunge ambao sisi wananchi ndio waajiri wao.

Kama inavyofahamika, moja ya majukumu ya mbunge ni kiunganishi kati ya wananchi na serikali kwa kuwasilisha kero za wananchi wa jimbo lake na kuzipeleka serikalini ili kupatiwa ufumbuzi. Jukumu linguine ni kutunga sheria mbalimbali ambazo zinaongoza nchi.

Mtu mwingine anaweza kujiuliza na pengine kunishangaa kwanini natumia muda wangu kufuatilia Bunge la 12 ambalo baada ya uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba, mwaka jana, kelele zilipigwa na wananchi kwamba litakuwa bunge lisilo na meno kwa sababu wabunge wengi wanatoka chama tawala.

Kuwa na wabunge wengi wa chama tawala ukilinganisha na Bunge la 11 lililopita ndicho hasa kinachonivutia kufuatilia ili kujiridhisha kama kweli litakosa meno kama ambavyo kelele zinapigwa huku mitaani.

Lakini ni jambo lililo wazi kuwa tangu Bunge la 12 limeanza vikao vyake, tumeshuhudia wabunge hususani wa kutoka chama tawala wakitoa hoja nzito za msingi na wakati mwingine kuibana serikali ili ifanye yale ambayo wananchi wanayataka.

Miongoni mwa wabunge ambao nilipenda sana kuwasikiliza kwa sababu tu wanajua jinsi ya kujenga hoja nzuri na zikaeleweka ni kijana wa jimbo la Bumbuli mkoani Tanga, January Makamba.

Mbunge huyu machachari nilianza kumfuatilia tangu alipoingia bungeni kwa mara ya kwanza baada ya kumng'oa aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo, Mzee William Shellukindo.

Jumatano wiki hii nilikuwa nafuatilia Bunge kwa mara nyingine alinifurahisha kwa jinsi alivyojenga hoja nzuri hususani suala la kwamba kila anayesifia jambo lililofanywa na aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dk. John Magufuli, basi anajipendekeza ili kuteuliwa labda uwaziri.

"Tusihukumiane... mtu anaposifu asionekane kuwa anataka cheo, anapokosoa asionekane kuwa ana nongwa na anapokaa kimya, asionekane kuwa amesusa," anasema January Makamba.

Kauli hii ya Makamba naweza kusema imeleta matumaini mapya na fikira pevu kwa sababu tangu utawala wa Hayati Magufuli na Rais wa sasa, kumekuwa kukijitokeza kauli kwamba kila unaposifia jambo lolote unaambiwa unajipendekeza ili upewe cheo.

Kauli hizi ambazo naweza kusema ni za kijinga, zimekuwa zaidi zikisemwa na wapinga maendeleo ambao hakuna hata jambo moja kwao wanaloliona limefanywa na serikali ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Mimi kwangu nasema Makamba yuko sahihi kabisa kwani hata maneno kama mabeberu, vibaraka wa mabeberu, wapinga maendeleo, maadui wa taifa sasa iwe basi. Yabaki kuwa historia kwani yanaligawa taifa letu.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA,**
**MUNGU LIBARIKI BUNGE**

**Kwa maoni na ushauri tumia barua pepe mwanakatwe2015@gmail.com**

## DARASA LA NDOA



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

**Ni muhimu vijana watumie ujana wao vizuri kwa kuweka msingi na mazingira bora ya maisha yao ya baadaye. Waingereza wanasema, Choices you make in life make you. Hii ni kusema hali aliyonayo mtu ni matokeo ya uamuzi alioufanya na anavyotumia muda wake**

# ATHARI ZA KUISHI KINYUMBA KABLA YA NDOA KWA VIJANA

SIKU hizi kuna wimbi kubwa la vijana wa kike na wa kiume wanaoishi kinyumba kabla ya ndoa. Miongoni mwa vijana hao ni wanafunzi katika vyuo mbalimbali hasa vile vya eli9mu ya juu.

Uhaba wa hosteli za kulaza wanafunzi katika vyuo vingi umechangia hali hii. Wako baadhi ya wanafunzi ambao wameamua kupanga vyumba na kuishi kama mume na mke.

Sambamba na hii, wako baadhi ya mabinti (vivuruge) wenye uhusiano wa kimapenzi na kinababa wenye familia zao (sugar daddies), ambao wamewapangishia vyumba vya kuishi. Vijana wanaona kuishi hivyo ni jambo la kawaida na wazazi wengi hawajui kinachoendelea katika maisha ya watoto wao.

Hali hii huchangia vijana wengi kutokufanya vizuri katika masomo yao kwa kuwa suala la mapenzi huchukua nafasi kubwa zaidi kuliko masomo. Uongozi wa vyuo vingi haufuatilii sana mambo haya kwa kuamini kuwa vijana wanaojiunga na vyuo ni watu wazima, wanaojitambua na wenye kujua namna ya kujitawala. Hata hivyo, hali halisi ilivyo ni kinyume na matazamio hayo.

Vijana wengi ni wahanga wa mahusiano na athari zake ni kubwa sana katika maisha yao. Miongoni mwa athari zitokanazo na kuishi kinyumba kabla ya ndoa ni;-

- Hupunguza thamani na heshima.
- Kupoteza ladha na nguvu za maumbile.
- Kuchakaa na kuchoka mapema. Vijana wengi wamepoteza fursa ya kufurahia ujana wao kwa sababu ya kuzeeka kabla ya wakati.
- Uwezekano wa kuvunjika kwa uhusiano wakati wowote ni mkubwa. Utafiti mbalimbali unaonyesha kuwa uhusiano unaojengwa katika msingi wa ngono hudumu kwa muda mfupi. Hali hii husababisha matatizo ya kisaikolojia na ongezeko la wagonjwa wa afya ya akili.
- Kujengeka kwa tabia ya kutokudumu katika uhusiano na kuishi maisha ya vinyongo na visasi. Wako ambao wamewachukia wanaume au wanawake kwa sababu ya kujeruhiwa kimapenzi.
- Kujengeka kwa hali ya kutokupenda kuoa na kuolewa kwa sababu ya uzoefu wa maisha ya uhusiano wenye maumivu ambayo mtu ameyapitia.
- Kujengeka kwa tabia ya kutokupenda kubeba majukumu na kutokuwajibika (lack of commitment). Tatizo hili linawakabili zaidi vijana wa kiume kuliko wa kike.
- Kutokea kwa mimba zisizotarajiwa (unplanned pregnancies) na vitendo vya ukatili wa kijinsia. Waathirika wakubwa hapa ni vijana wa kike. Ni muhimu mabinti wajiepushe kuwa wamachinga wa miili yao.
- Vijana kuwa baba na mama bila kutarajia na pasipo maandalizi. Hiki ni chanzo kimojawapo cha ndoa za mapema (early marriages) na kuzalisha wazazi wasiojitambua. Mahali pengine, hali hii imeongeza umaskini na hali duni ya maisha kwa kijana mwenyewe na familia anayotoka.
- Kujengeka kwa tabia ya tamaa na kupenda ngono (addicted), hali inayosababisha vijana wengi kukosa uaminifu katika uhusiano.
- Vijana kujiweka katika hatari kubwa (at high risk) ya kupata magonjwa hatarishi na ambukizi kama vile UKIMWI, kaswende na kifua kikuu (TB).
- Kuongezeka kwa vitendo vya utoaji wa mimba, hali ambayo imesababisha baadhi ya mabinti kutokushika mimba na kutokupata watoto baadaye (ugumba).
- Kuondoka katika kusudi au lengo na kupoteza mwelekeo wa maisha (direction).
- Kupoteza nguvu kazi yenye afya bora na imara.

**Hitimisho**

Maisha ya ujana ni zawadi ambayo mtu anapewa na Mungu mara moja katika maisha yake ("only once in a life time"). Hii ndiyo kusema kuwa ujana ni kipindi cha mpito. Ujana ukipita haurudi tena! Kwa mantiki hii, kijana akiukosea ujana wake leo ni sawa kwamba ameikosea baadaye au kesho yake kwani chochote anachofanya mtu wakati wa ujana, ni taswira (reflection) ya maisha yake ya baadaye.

Ni muhimu vijana watumie ujana wao vizuri kwa kuweka msingi na mazingira bora ya maisha yao ya baadaye. Waingereza wanasema, Choices you make in life make you. Hii ni kusema hali aliyonayo mtu ni matokeo ya uamuzi alioufanya na anavyotumia muda wake.

Kwa mantiki hiyo, vijana wasiwe na haraka ya maisha kwa kuwa maisha ukiyaharakisha, yatakuharakisha. Kila jambo lina majira yake, hivyo, vijana wajifunze kutumia vizuri ujana wenu kwa mambo yenye faida.

Ujana wako ufanyike baraka kwako mwenyewe, wazazi wako, jamii na taifa. Nafasi ya kijana katika taifa ni ya pekee sana. Taifa lenye nguvu ni lile linalowekeza kwa vijana.

**Mungu ibariki Tanzania!**

**Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online.**

**Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**

MAISHA
MEI 2, 2021
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili



Ukurasa 10

**Baba yuko bize, watoto nao wamsahau**



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**

Dondoo wakati wa kuchagua rangi za kuta za nyumba yako



**HARUSI**

Ukurasa 12



**MAFUTA YA UFUTA**

# Siri ya urembo uliojificha

Ukurasa 14

# Baba yuko bize, watoto nao wamsahau

Na Beatrice Moses

HIVI karibuni nilifanikiwa kutazama video fupi kwenye moja ya mtandao wa kijamii.

Kilichoonyeshwa kwenye video hiyo ni baba, mama na watoto wawili wakiwa wamesimama, kisha kuna sauti inawaamuru wazazi hao kila mmoja akimbilie upande wake.

Wakati huo baba alikuwa amesimama upande wa kushoto, na mama upande wa kulia na watoto wote wakiwa wamesimama kati yao. Kilichotakiwa kufanyika hapo ilikuwa ni kila mzazi akimbilia upande wake ili ibainike watoto watakimbia kwa kumfuata nani. Hatua hiyo ilirudiwa mara tatu, awali mara zote mbili watoto walikimbia kwa kufuata upande aliokimbilia mama yao, hali hiyo ilimshawishi baba kuwanyakua watoto na kukimbia nao upande wake huku akiwa amewabeba.

Ni wazi kwamba kwa kufanya hivyo baba yule alikuwa amefanya makosa kwenye kipimo kile ambacho kilihitaji kufahamu ni namna gani watoto wapo karibu



na mzazi yupi pale inapotokea tatizo.

Yawezekana baadhi ya watu waliyotazama video hiyo waliichukulia kwa mtazamo tofauti kulingana na mazingira wanayoishi au waliyokulia, ila ni wazi kwamba iwapo utafiti huo ungefanywa kwenye kila familia yenye watoto wanaoishi na wazazi wote wawili, watoto wengi wangekimbilia upande wa mama zao.

Kinababa wengi licha ya kujitahidi katika kuhakikisha watoto wao wanapata huduma zote muhimu ikiwamo chakula, kulipa ada na kuwanunulia nguo, bado watoto wanahitaji uwepo wao na ukaribu katika makuzi yao.

Kuna akina baba wachache ambao wametenga muda wa kuwa na watoto wao, ikiwamo kuwapeleka kutembelea sehemu mbalimbali za vivutio.

Ni kawaida kuwaona akinamama wakitenga muda wa kucheza na watoto iwe ni muziki au michezo mingine kama vile kuruka kamba ama mpira, au kuongozana nao kwenda kununua mahitaji mbalimbali.

Ni vyema wazazi wa kiume kukumbuka kuwa suala la kushiba , kwenda shule na kupatiwa huduma nyingine muhimu ambazo zinahitaji gharama fulani siyo kichocheo kwa mtoto kuna ukaribu wa baba japo ni wazi kuwa huduma hizo ni muhimu.

Jambo baya zaidi ni kwamba wakati mwingine mahitaji hayo yote yanapitia mikononi mwa mama hivyo watoto huamini kuwa baba ndiyo kila kitu kitu kwao, ni vizuri kutenga muda wa kuzungumza na watoto, kuongazana nao madukani wakati wa kununua mahitaji.

Yawezekana kuna baadhi ya kina baba wanashindwa kuwa karibu na watoto kwa sababu ya kubanwa na majukumu, ni vizuri muda wako mchache wa kupumzika ukajitahidi kuweka japo nusu saa au saa nzima ya kuzungumza ama kucheza na watoto wao ili kuimarisha upendo wako na wao.

## NA HAMIS KIDAGO 0657 207168 QUIZ

**L'Adjectif Qualificatif – Vivumishi vya sifa**

**• Geuza vivumishi vya sifa vifuatavyo ambavyo viko katika jinsia ya kiume au masculin kwenda jinsia ya kike au féminin.**

**Mfano –** Jeune – jeune
• Grand – ..............................
• Brun – ..............................
• Distingué – ........................
• Charmant – ..............................
• Privé – ....................................
• Tranquille – ..............................
• Fragile – ....................................
• Solide – ......................................
• Lourd – ......................................
• Confortable – ..............................
• Petit – ..........................................
• Joli – ..............................................
• Original – ....................................
• Agréable – ..................................
• Content – ......................................
• Connu – ......................................

**Muhimu:** Vivumishi vya jinsi ya kiume vinavyoishia na herufi ehubadilika kuwa vya jinsia ya kike kwa kuongeza herufi e nyingine. Ingawa sio kwa maneno yote. Mfano distingué (masculin) – distinguée (féminin) lakini tranquille (masculin) na tranquille (féminin).

**• Chagua jibu sahihi kutoka kwenye mabano.**

**Dans la cuisine**
• C'est un repas (froid – froide).
• Attention! l'assiette (fs) est (chaude – chaud).
• Cette viande est très (salé – salée).
• C'est une sauce (sucré - sucrée)?
• Le gâteau est trop (cuit - cuite).
• La cuisson est (parfait - parfaite).
• Le jus d'orange est (glacé - glacée).
• Voici une salade (verte - vert).
• C'est un plat (épicé - épicé).
• Cette recette est (excellent - excellente).

**• Weka jibu sahihi kutoka kwenye mabano.**

**J'ai dessiné…**
• Une maison (gris - grise).
• Le ciel (bleu - bleue).
• La pelouse (vert - verte).
• Un oiseau (noir - noire).
• Un arbre très (haut - haute).
• Et un (grand - grande) soleil.


**• Chagua kutoka kwenye mabano neon sahihi.**
• Une journaliste (espagnole - espagnol).
• Un artiste (japonais - japonaise).
• Un photographe (allemande - allemande).
• Une rédactrice (chinois - chinoise).
• Un dessinateur (polonaise - polonaise).
• Une correspondante (mexicaine - mexicain).
• Un reporter(argentin - argentine).
• Une actrice (américain - américaine).

**• Geuza maneno yafuatavyo kuwa katika jinsi ya kiume umoja.**

**Mfano:** une rue étroite – un chemin étroit.
• Une place animée – Un parc.................
• Une grande avenue – un ........... boulevard.
• Une entrée large – un troittoir.....................
• Une place tranquille – un jardin........................
• Une petite impasse – un ...................... passage.
• Une rue agréable – un quartier..........................

## WATOTO

# PAKA RANGI



CHEKA



Alichokifanya daktari

MAZUNGUMZO kati ya marafiki wawili yalikua kama ifuatavyo;

**Juma:** Habari yako kijana?

**John:** Safi tu nambie.

**Juma:** Aiseee! muda kweli naona unaangaika na bodaboda tatizo nini kwani?,

**John:**Nafuta kuni zinazosababisha moshi, lakisi sizioni

**Juma:** Ooohhhh! Kweli huyu mzima!

**SWALI**

Zao la mwani linalimwa sehemu gani?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Mchumba anatoka na rafiki yangu, sasa nimechanganyikiwa, nifanyeje?

***KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na vituko vya Maisha Ndivyo Yalivyo . Leo nitupie macho anga la vijana. Hili ni kundi muhimu sana katika ujenzi wa taifa. Pamoja na ukweli huo, vijana wengi wamenaswa katika eneo la uhusiano na hawajui chanzo chake.***

Vyanzo ni vingi. Hebu nijikite zaidi kwenye eneo hilo la uhusiano kwa maana ya marafiki. Kabla sijaendelea, sikia ujumbe huu mfupi toka kwa msomaji wetu aliyeniandikia kupitia simu ya kiganjani akitaka ushauri.

“Mama mimi ni binti umri miaka 19. Tatizo langu ni kwamba ninaye rafiki yangu wa kike nimegundua anatoka na mchumba wangu. Nimenasa mawasiliano yao kwenye simu ya mchumba wangu.

“Sasa nikimwuliza mchumba wangu kwa nini anafanya hivyo, anakataa kwamba si kweli. Mchumba huyu hajatulia, ijapokuwa nimewekeza sana kwake. Hata mama yake mzazi namsaidia sana kwa kumnunulia vitu na kadhalika.

“Isitoshe, nimeshajiwekea malengo mengi ya kimaisha na kijana huyu kwamba ndiye mume wa ndoto yangu. Kwa hiyo nimechanganyikiwa sijui nifanyeje. Naomba ushauri.” Hivi ndivyo anavyomaliza ujumbe wake msomaji huyu.

Hakika, yuko kwenye wakati mgumu hasa ikizingatiwa kuwa amedhamiria kuolewa naye. Ilibidi nimpigie simu nikaongea naye kwa kirefu. Katika kumdadisi akaniambia tatizo lingine kwamba takriban miezi miwili hajapata hedhi, hali inayompa wasiwasi. Kwa hili nilimshauri aende hospitalini akapime ajiridhishe kama ni ujauzito au la.

Msomaji wangu, hebu sasa nieleze kidogo kuhusu urafiki kwa maana ya faida na hasara zake. Maneno ya upole humwongezea mtu marafiki, kuongea kwa adabu husababisha hisani. Yakupasa uwe na marafiki wengi wa kukusalimu lakini wa kukushauri, awe mmoja tu kati ya elfu.

Ukitaka kupata rafiki mpime kwanza, usiharakishe kumwamini. Maana kuna rafiki aliye rafiki inapomfaa; siku ya taabu hatakuwako kukutegemeza. Pia kuna rafiki abadilikaye kuwa adui, atazusha ugomvi ili kukuaibisha.

Pia yuko rafiki ambaye ni rafiki wakati wa mlo, lakini siku ya taabu hatakuwako kukutegemeza. Ukipata fanaka atajifanya sawa nawe na kuwaamuru watumishi wako. Lakini ukifilisika atakugeuka na kujificha mbali nawe. Ni muhimu ukae mbali na adui zako na pia ujihadhari na rafiki zako.

Ukiacha hao marafiki wabaya, wako marafiki waaminifu ambao mtu anapaswa kuwa nao. Rafiki mwaminifu ni kinga imara na ampataye kama huyo, amepata hazina. Rafiki mwaminifu ana thamani kuliko chochote, hakuna awezaye kupima ubora wake.

Rafiki mwaminifu ni dawa itiayo nguvu mwilini, watu wamchao Mungu hupata marafiki wa kweli, maana alivyo mtu ndivyo na rafiki zake. Pamoja na yote hayo, neema ya Mungu ndiyo impayo mtu marafiki sahihi.

Mpenzi msomaji, nimejaribu kueleza aina za marafiki ili yale wanayopitia vijana wetu katika eneo la mahusiano wajitafakari. Hiyo ni vita. Usipojua upo kwenye vita gani, huwezi kushinda. Binti ninayemjadili yuko vitani lakini hajitambui. Anadhani yuko peke yake kumbe sivyo. Tayari amejua rafiki karibu anatoka na mchumba wake. Sasa anaomba ushauri, ushauri afanyeje?

Tatizo la vijana wengi wanakurupuka kupata marafiki pasipo kuwapima kwanza. Wanaharakisha kuwaamini kumbe baadaye ni majanga. Angalia binti huyu anaye rafiki wa kike waliyeshibana lakini sasa ndiye anayemsaliti kwa kuingilia uchumba wake.

Anapaswa kujua kuwa adui wa mtu ni wa nyumbani kwake. Ni yule aliye karibu siyo wa mbali. Tazama tatizo lingine la binti huyu anahisi kuwa na ujauzito. Sasa itokee na huyo shoga naye abebe ujauzito , hilo sakata litakuwaje? Nimesema mara nyingi kuwa shetani hutumia watu kuharibu hatma za wengine.

Inawezekana kijana naye ametekwa ufahamu na huyo rafiki wa mchumba wake. Kama kweli uhusiano upo, anatambua tabia hiyo siyo sawa lakini hawezi kutoka, hawezi kuachana nayo.

Msomaji wangu, nijuavyo mimi ni kwamba, sifa na aibu vyote hutokana na kusema. Ulimi wa mtu waweza kumwangamiza. Usikubali kujipatia sifa kwa kuteta, usikubali kusema kitakachohatarisha wengine maana kama vile aibu imjiavyo mwizi, ndivyo hukumu kali itakavyompata mdanganyifu.

***Msomaji, kwa leo niishie hapa. Wiki ijayo nitamwelezea binti mwingine ambaye marafiki walimpotezea kwenye madanguro, sasa anajuta, anatamani kuokoka. Je, una maoni, kisa cha maisha? Tuma ujumbe kupitia 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Siku ya uhuru wa habari iambatane na mabadiliko

KILA Mei 3, waandishi wa habari, wamiliki na wadau wa vyombo vya habari duniani huungana kuadhimisha siku hiyo kwa kaulimbiu tofauti tofauti.

Kwa mwaka huu, maadhimisho hayo yanafanyika kitaifa mkoani Arusha, chini ya kaulimbiu ya ‘Habari kwa Manufaa ya Umma’ ambayo inataka uwajibikaji kwa kila mmoja kuhakikisha habari zinapatikana na kuwafikia wananchi.

Ni muhimu sana habari zikawafikia wananchi kwa wakati kwa kuwa ni haki yao kujua na kuona uwajibikaji wa viongozi wao, mapato na matumizi ya fedha za mipango mbalimbali na utekelezaji wake.

Katika maadhimisho hayo ambayo yatawaleta pamoja wadau mbalimbali, mada zitakazojadiliwa ni ukuaji wa vyombo vya habari na uhuru, maendeleo ya watu kama mtaji; mazingira ya kisheria, sera na ufanyaji kazi; na vyombo vya habari na masuala ya kidigitali.

Maadhimisho haya yanafanyika kukiwa na utashi wa kisiasa kutoka kwa kiongozi mkuu wa nchi, Rais Samila Suluhu Hassan, ambaye ameagiza kufunguliwa kwa vyombo vya habari vilivyokuwa vimefungiwa, ikiwamo kuwapo kwa uhuru wa kujieleza, ingawa bado kuna magazeti yaliyokuwa yamefungiwa tangu serikali ya awamu ya tano yako kifungoni.

Pia ndiyo mwaka ambao muda wa msamaha wa miaka mitano uliotolewa kwa waandishi wa habari kujiendeleza kitaaluma kuwa na diploma unakwisha.

Licha ya mafanikio mengi yaliyofikiwa, bado taaluma ya uandishi wa habari inakabiliwa na kero nyingi, ikiwamo sheria ambayo bado ina vifungu ambavyo vinakwaza utekelezaji wa majukumu ya kila siku.

Mathalani, sheria imempa mamlaka waziri kuteua wajumbe wa bodi ya ithibati ambayo itasimamia taaluma ya habari, lakini pia leseni za vyombo vya habari zinahuisha kila mwaka.

Madhara yake ni kwamba kwa chombo cha habari ambacho kinakosoa sana kiko hatarini kukosa leseni iwapo habari zake zitakuwa zimemgusa Waziri au wanaohusika au hata serikali kwa ujumla.

Pia kosa la kitaaluma linaadhibiwa kama kosa la jinai kwamba kuna faini au kifungo, na iwapo busara ya hakimu itamwongoza, basi ataamua kutoa vyote kwa wakati mmoja.

Bado tasnia ya habari waajiriwa wake wanakabiliwa na kero nyingi ikiwamo maslahi duni, kukosa bima za afya na mikataba ya ajira kulingana na taaluma zao.

Tanzania ni moja ya nchi zilizoridhia sheria ya haki ya upatikanaji wa taarifa, ambayo inalazimisha mamlaka kutoa taarifa na yule anayenyimwa taarifa kushtaki, lakini bado kutoa taarifa imekuwa kero kubwa.

Sheria inaelekeza mwandishi kujaza fomu na kuambatanisha maswali yake kwa mhusika na hiyo imetumika kama mbinu ya kuficha taarifa kwa kuwa wengi licha ya kuandikiwa bado ushirikiano umekuwa mdogo na huishia kutoa habari wanazotaka na kuacha maswali yanayoulizwa ambayo wakati mwingine ni kwa manufaa ya umma.

Kaulimbiu ya kuwa habari ni kwa manufaa ya umma, hivyo inapaswa kuishi kwa kila mmoja kwamba haipaswi kufungia habari bali kuitoa ili jamii ijue nini kinafanyika katika ngazi mbalimbali.

Uwazi na uwajibikaji serikalini ni muhimu kwa manufaa ya wananchi kwamba wananchi watajua kodi zao zinatumikaje kwa manufaa yao, watafanya uamuzi wa aina mbalimbali, watapiga hatua kimaendeleo kutokana na kwamba wana taarifa sahihi kwa wakati sahihi.

Aidha, maadhimisho haya yanafanyika katika kipindi ambacho upashanaji habari umebadilika kutokana na kasi ya ukuaji wa teknolojia, kwamba sasa wananchi nao ni waandishi wa habari wasio rasmi, huku wenye taaluma yao wakitakiwa kuongeza thamani katika kilicholetwa na wananchi ambao hubeba kila kitu pasipo kuangalia maadili ya taaluma.

Pia tatizo la upatikanaji wa matangazo, ambayo yamepungua kutokana na uwapo wa mitandao ya kijamii, kiasi cha vyombo vya habari kutakiwa kuwa na ubunifu wa kuongeza mapato badala ya kutegemea matangazo pekee.

Lakini jinsi gani matangazo yanaweza kutumika kama fimbo ya kuiumiza sekta ya habari, kwa kuwa habari wakati mwingine huwagusa watangazaji, na kama ilivyoelezwa kuwa ni mali umma maana yake unapaswa kupata kila ambayo imekidhi matakwa ya kitaaluma.

# HARUSI







Familia ya David Matovu wamekuwa na furaha ya aina yake baada ya kijana wao, Cathbert David Matovu, kufunga ndoa na Paulina Kalokola Aprili 17, katika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Mabibo Extenal, kisha sherehe ya kuwapongeza iliyofanyika kwenye Ukumbi wa JKT Mwenge, Dar es Salaam.





# MITINDO



TUPIA KISASA

# Mwezi wa Ramadhan

MWEZI wa Ramadhan unazidi kuyoyoma, kila muumini wa Kiislam anatekeleza nguzo hiyo muhimu katima imani yao. Pamoja na kujizuia kunywa na kula, lakini katika kipindi chote cha mfungo vazi la kujistiri mwili linazingatiwa.

Baadhi wanawake uhangaika katika kupata mavazi ambayo licha ya kuwatoa tofauti, liwe linakidhi matakwa ya imani yao kwa kuhifadhi vyema mwili.

Hata hivyo, kuna baadhi ya mavazi ambayo unaweza kusema ya kisasa zaidi, lakini unaweza ukayabadilisha kuendana na mwezi huu bila kutumia gharama nyingi.

Haya ni baadhi tu ya mavazi ambayo unayo na unaweza kuvaa katika kipindi hiki cha mfungo.

**VAZI LA TUXEDO**

Kama unayo basi ni msaada mkubwa kipindi hiki cha mwezi wa Ramadhani, unaweza kuivaa koti lako la Bleza, pia ndani unapigilia shati, huku chini ukiwa na suruali au sketi ndefu.

**VAZI LA 'TURTLE NECK TOP'**

Nguo za aina hii znapendwa sana, ukiwa nayo itakusaidia katika mwezi huu, unaweza kuvaa na sketi ndefu, suruali na hata gauni lenye mikono mifupi, jambo zuri vazi hili unaweza ukafunga kiremba kichwani ili kustiri kifua na shingo.

**VAZI LA 'CULOTTES PANTS'**

Hizi ni zile suruali pana kwa chini ni kama fupi hivi, zina raha ukivaa na idadi kubwa ya wanawake wanayo.

Nguo hizi unaweza kuzivaa na fulana ya mikono mirefu huku ukitupia na mtandio.

UREMBO



MAFUTA YA UFUTA

# Siri iliyojificha

UFUTA ni chakula au kiungo kinachopendwa na watu wengi kutokana na ladha yake tamu na harufu murua.

Zao la ufuta linapatikana sehemu nyingi za Tanzania, hivyo ni rahisi watu kutumia kama chakula kwa kutengeneza kashata au kiungo endapo utasangwa na kuwa unga.

Hata hivyo, kuna idadi kubwa ya watu hawajafahamu kwamba mafuta yanayotokana na ufuta yanatumika katika suala zima la urembo, hasa kuboresha afya ya ngozi, kung'arosha midomo na kuimarisha nywele.

Zifuatazo ni faida za mafuta katika matumizi ya urembo.

**MAFUTA YA UFUTA NA NGOZI**

Mafuta ya ufuta yana vitamini ambayo hufanya ngozi kuwa safi na kujikinga na maambukizi ya magonjwa mbalimbali..

Wataalamu wanasema mafuta hayo ni moja ya mafuta asili yenye uwezo mkubwa wa kutibu weusi shingoni na chini ya macho, pia kupambana na tatizo la chunusi.

**FAIDA YA MAFUTA YA UFUTA KATIKA NYWELE**

Mafuta haya yana asilimia kubwa ya vitamini ambayo inakuza nywele haraka, kuzuia kukatika na kung'arisha.

Unapopaka mafuta ya ufuta huzuia ukavu wa nywele pamoja na kulainisha nywele. Pia

Inasemekana kuwa mafuta ya ufuta yana uwezo wa kuongeza weusi nywele na hupambana na mvi.

**UREMBO WA MIDOMO**

Mafuta ya ufuta hung'arisha meno pale unapopaka na pia huipa nguvu fizi.

Faida nyingine ni pamoja na kuua bacteria hatari mdomoni na kuzuia harufu mbaya.







MAPISHI

Na Mary Geofrey



# Utamu wa visheti

LEO katika safu ya mapishi tunajifunza namna ya kupika visheti au kwa jina la vikokoto.

**MAHITAJI**

Unga wa ngano kilo moja na nusu, siagi iliyoyeyushwa vijiko viwili vya chakula, maziwa robo lita au kikombe kimoja cha maji, chumvi na mafuta ya kupikia lita moja na nusu.

**MAHITAJI YA SHIRA NYEUPE**

Maji kikombe kimoja, sukari nusu na robo, kifuniko kimoja cha Vanilla na hiliki punje 10.

**JINSI YA KUANDAA VISHETI**

Yeyusha siagi, kisha weka unga wa ngano kwenye bakuli kubwa na uchanganye na siagi iliyoyeyushwa.

Mimina maziwa baridi kidogo kidogo kwenye unga au maji ya baridi na changanya.

Anza kuchanganya changanya unga na maziwa baridi mpaka utengeneze donge kama la chapati Usikande ila changanya kawaida. Gawanya donge la unga sehemu tatu, sukuma donge moja moja kwa shape ya chapati nene, kisha tumia kisu kukata chapati kwa urefu.

Baada ya kukata kwa urefu, malizia kukata kwa shape ya visheti saizi ndogo ndogo.

**KAANGA VISHETI VYAKO**

Weka mafuta ya kupikia kwenye karai, acha yachemke, kisha tia vipande vyako vya visheti kwenye mafuta ya moto,weka vipande vichache visibanane sana.

Baada ya dakika 5 geuza visheti, kaanga upande wa pili mpaka viwe brown. Baada ya hapo toa visheti weka kwenye chombo kinachochujisha mafuta.





**KUANDAA SHIRA NYEUPE**

Chukua sufuria kubwa, weka sukari, maji na vanilla na hiliki na acha mchanganyiko uchemke kwenye moto mdogo mpaka sukari iyeyuke kabisa na cha ichemke hadi iwe nzito.

Shira nyeupe ukiwa tayari, basi chukua visheti vyako ulivyokaanga changanya kwenye shira ikiwa bado ya moto, koroga koroga hadi visheti vikolee na unaweza changanya visheti kidogo kidogo ili shira ishike vizuri.

Ili visheti vitoke vizuri hakikisha shira haipoi, ikipoa iweke kwenye moto kidogo ndo uendelee kuchanganyia kwenye visheti.

Visheti vyako vitakuwa tayari kwa kuliwa na chai, soda au juisi au kula Kama kichangamsha kinywa wakati unaendelea na shughuli zako.

Visheti pia vinafaa kula wakati huu wa mfungo wa ramadhani.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya

# Namna ya kupanga kabati la vyombo kwa urembo wa nyumba yako







KABATI la vyombo ni miongoni mwa samani zenye uhitaji mkubwa kwenye nyumba.

Watu waliobarikiwa kujenga au kuishi kwenye nyumba zenye nafasi za kutosha, kabati huwa ni miongoni mwa vitu muhimu kwao kwa ajili ya kuhifadhia vyombo.

Lakini leo nataka tuzungumzie kazi nyingine ya kabati kwenye eneo la urembo katika nyumba. Kama ilivyo urembo mwingine kwenye nyumba, kabati la vyombo nalo lina nafasi ya kutumikia kama urembo.

Kutumika kwa kabati kama urembo si kwa kuweka maua au urembo mwingine ndani yake, ni kwa kutumia vyombo hivyo hivyo ambavyo badala ya kutumika kwa ajili ya matumizi ya chakula, pia vitumike kama urembo.

Na ili vitumike kama urembo, kitu cha kwanza lazima tujue eneo linapopaswa kuwekwa ndani ya nyumba husika.

Jambo lingine lazima kuhakikisha kwamba vyombo vinavyowekwa kabatini ni vile vyenye mvuto au vizuri. Usichukuea tu vyombo ilimradi na kwenda kuviweka humo.

Hakikisha unazingatia rangi za vyombo vyako vinavyowekwa kabatini, zisiwe zile za kuumiza macho sana na ikiwezekana rangi zisipishane sana na zile za vitu vyote vilivyomo kwenye nyumba yako.

Kuwa mbunifu kuvipangilia kwenye kabati ili vilete mvuto, zingatia aina na muundo wa vyombo.

Kama ni sahani, hakikisha unapangilia kuanzia zile kubwa kuelekea ndogo zake. Fanya hivyo na kwa glasi, vikombe, bakuli na vinginevyo ambavyo ni vizuri unavyokuwa umeviandaa kwa ajili hiyo.

Kumbuka si lazima viwe vinatumika, vinaweza kuwa maalum kwa urembo tu na vile vya kutumia ukaviweka sehemu nyingine au katika kabati la juu la jikoni.

Na kama uwezo hauruhusu, unaweza pia ukavitumia, lakini unapomaliza hakikisha unavisafisha vizuri na kuvirudisha katika sehemu yake vinapopangiliwa na katika hili ubunifu zaidi unahitajika.

Katika mpangilio, unaweza kuamua glasi zikae sehemu yake, au ukaamua kila shelfu zikae tatu au nne kwa mpangilio mzuri au kila aina ya chombo ulicho nacho ukakitumia kwa mpangilio maalum katika shefu zote ili 'kunogesha zaidi'.

## Dondoo wakati wa kuchagua rangi za kupaka kuta za nyumba

**1:** Hakikisha rangi unayotaka kupaka kwenye kuta inacheza na hisia za mahali husika hasa kwa kuzingatia rangi za msingi.


**2:** Angalia ubora wa rangi kama ni nyepesi au nzito kutoka kwenye jamii ya rangi hiyo.

**3:** Pata ushauri kutoka kwa wataalamu wa rangi wakushauri aina gani unaweza kupaka katika kuta ili upate mwonekano mzuri zaidi.

**4:** Angalia kwa makini bajeti yako, ili gharama ya rangi isiwe juu na kusababisha baadhi ya kuta kukosa rangi au kupata hafifu.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2021
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
BINTI YANGU NI MJAMZITO... NANI KATI YENU ALIYEMTWISHA NIMPE ZAWADI.
ANGALIA SURA BABA UTAMJUA...
JIRANI NAONA TUNAELEKEA PABAYA NA MBUZI WAKO! KWA NINI WANAKULA MAZAO YANGU?
YAISHE! WAKIRUDI NITAWASEMA
VIPI MBONA UNAZODOA KAMA YANACHOMOKA!
UNGEJUA KAMA KODI YAKO NAITEGEMEA KWA NGUO ZA WATOTO NA SIKUKUU!!!
MWENZAKE NIKI-ZIDI SANA 'WIKI' NARUDI KWANGU KUJIOSHA..YEYE ANAGANDA!
MWEZI MZIMA UPO KWA KIMADA UNANIACHA NAHANGAIKA NA WATOTO!
MIMI NAKUPA BIA TU! SIKUPI HELA YA KULA NA WANAO KWAKO... SINA HIYO BAJETI
LABDA USIZIMIKE!
KAMA TUMEBWAGWA NA 'AKINA MAMA' TUSITANGAZE IBAKI KUWA SIRI YETU!
DOM
STAKI KUCHEKA KWA SASA MWENZAKO PRESHA IPO JUU...!
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...UMBEA HAUCHAGUI NENO ...

## HABARI PICHANI

# MAADHIMISHO YA SIKU YA WAFANYAKAZI DUNIANI



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akihutubia katika maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi), yaliyofanyika jana kwenye ukumbi wa Sheikh Idris Abdulwakil, Kikwajuni, Zanzibar. **PICHA: IKULU**



Wakulima wakipitisha bidhaa za kilimo mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Kenan Kihongosi (hayumo pichani), katika maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi), kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**




Wafanyakazi wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), wakiandamana wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wafanayakazi, katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Wafanyakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, wakiimba wimbo ya mshikamano wakati wa maadhimisho ya Mei Mosi, katika uwanja wa mpira wa Jitegemee, wilayani humo jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**




Baadhi ya Watumishi wa Ofisi ya Bunge, wakipita mbele ya jukwaa kuu katika maandamano ya Mei Mosi, kwenye Uwanja wa Jamhuri, jijini Dodoma jana. **PICHA: BUNGE**



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge (wa tatu kulia), akishiriki na wafanyakazi kutoka sekta mbalimbali za umma, kuimba wimbo wa mshikamano, wakati wa maadhimisho ya Mei Mosi katika Uwanja wa Jamhuri, jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

SAFU

MAKALA

# UPINZANI ULIO IMARA KAMWE HAUTAJENGWA NA WAHAMIAJI



Na Magabilo Masambu

**Kuna wakati vyama vya upinzani kwa kujua au kwa kutojua, vimeingia kwenye mtego huu wa kudhani kwamba wanaotoka CCM wana malengo ya kujenga upinzani wa kweli. Jambo hili limevigharimu sana vyama hivi kiasi cha baadhi ya viongozi kupewa mpaka dhamana ya ... kukupeperusha bendera zao ngazi ya urais na baada ya uchaguzi, unasikia "tumerudi nyumbani!"**

KAULI kwamba siasa ni maisha na maisha ni siasa inaweza kuthibitishwa kwa kutazama mienendo ya wanasiasa wenyewe katika kuhakikisha wanaitumia fani hiyo ili kufanikisha malengo yao.

Wako wanaosema kwamba umdhaniaye ndiye kumbe siye! Hili pia limejidhihirisha mara nyingi katika siasa zetu za Tanzania hasa miaka mitano iliyopita. Tumeona mengi kiasi cha kuona kumbe siasa ni jambo la uongo hivi na la kutowaamini wanasiasa.

Wakati tunaingia katika mfumo wa vyama vingi mwaka 1992 na kufanya uchaguzi wa kwanza mwaka 1995, vyama vingi vya upinzani havikuwa na namna ya kuwapata watu wapya zaidi ya wale waliogawanyika kutoka Chama Cha Mapinduzi (CCM). Ilikuwa kazi ngumu kuwapata wanasiasa ambao hawakutokana na chama kimoja kilichokuwapo kabla ya vyama vingi.

Tutakumbuka Augustino Mrema na NCCR yake alivyotikisa mwaka 1995. Lakini hata wagombea wa vyama vingine lilikuwa zao la CCM kiasi cha kufikirika kwamba inawezekana CCM walifanya janja ya kugawanyika ili kuwaridhisha tu wahisani waliotoa masharti ya kuwapo mfumo wa vyama vingi. Pia inawezekana ulikuwa mpango wa CCM kufanya hivyo kwa mkakati jambo ambalo mpaka leo linaonekana kama liko hivyo japo laweza pia lisiwe hivyo.

Kuna wakati vyama vya upinzani kwa kujua au kwa kutojua, vimeingia kwenye mtego huu wa kudhani kwamba wanaotoka CCM wana malengo ya kujenga upinzani wa kweli. Jambo hili limevigharimu sana vyama hivi kiasi cha baadhi ya viongozi kupewa mpaka dhamana ya kukupeperusha bendera zao ngazi ya urais na baada ya uchaguzi, unasikia "tumerudi nyumbani!"

Kauli ya siasa ni maisha inaonekana kuthibitika kwamba inawezekana wanasiasa wanaohamahama vyama wapo katika kuhakikisha wanakipata kile wanachokitafuta. Bahati mbaya ama wanakosa uvumilivu huko wanakoelekea au unakuwa mpango mahsusi wa kule wanakotoka hakuna anayejua bali wanaojua ni wenyewe na bahati mbaya pia hatujawahi kusikia wakisema yale watu wanayodhani ndiyo sababu ya kuhamahama kwao. Hata wale wanaotoka upinzani na kwenda CCM pia sababu zimekuwa hazieleweki wengine wanasema maneno mawili tu "Nimerudi Nyumbani" bila kujibu kwa nini umerudi!

Si jambo baya upinzani au hata CCM yenyewe kuwakaribisha wanachama wanaotoka vyama vingine, angalau kwa CCM kwa sababu ya ukomavu na kuwa na ziada kubwa kwenye chama. Wale wanaohamia wanawatumia kwa malengo na baadaye kuwaweka pembeni, lakini kwenye upinzani wao wanaona hao wanaohamia kama fursa kitu ambacho kitawarudisha nyuma miaka na miaka.

Tunahitaji upinzani imara kama kichocheo cha maendeleo. Hata leo nikiwa kwenye chama chochote kitakachotawala, kiwe ni CCM au CHADEMA, kwa fikra na maono yangu juu ya vyama mbadala, bado nitahitaji chama kizuri mbadala wa kile kilichoko madarakani kuwa imara ili kilichoko madarakani ama kisilale au kuwa na kiburi kwa wananchi.

Baadhi yao wanaondoka upinzani tena kwa kunukuu baadhi ya vifungu vya Biblia na wakati waliohamia katika vyama hivyo pia walinukuu vifungu hivyo, unaweza kuona namna gani inavyoshangaza. Jambo hili linaleta picha mbaya katika siasa kufikia kiasi cha kuona kwamba ili uwe mwanasiasa mzuri Tanzania inakulazimu uwe mnafiki, muongo, mzandiki na mambo mengine mabaya.

Kwa sababu siasa ndiyo inayoamua maisha ya watu, haikupaswa kuwa na sura hii ambayo baadhi ya wanasiasa wanajaribu kuionyesha. Sababu za mtu kuhama chama zinatakiwa ziwe za kihitikadi na si kwa sababu uliko wameshindwa kukutimizia matakwa yako.

Kinachotokea wanaokupokea wakiwa na akili watakupokea kisha utawekwa pembeni japo wakati mwingine inalazimika wakupe nafasi kama kichocheo cha kuwafanya wengine pia watoke ulikokuwa lakini si kwamba unapendwa sana unaweza kuwa hata balozi au mbunge wa kuteuluwa. Kama alivyowahi kusema Hayati John Pombe Magufuli kwamba bado utakuwa umekatwa mkia, hivyo ng'ombe wengine zizini wanakushangaa.

Ni karibu miaka 30 ya mfumo wa vyama vingi, hivyo ni wakati wa vyama vya upinzani kuwatumia vijana wao zaidi kwenye nafasi nyeti kuliko kuendelea kukopa majembe ya CCM na baadaye yanakwenda kulima nyumbani kama ambavyo mama amesema wakati akimpokea Lazaro Nyarandu juzi Dodoma kwamba "Nyumba uliyoizoea kuihama taabu hata wanaume wanajua."

Tujifunze kwa nchi zingine duniani ni aghalabu kusikia mwanasiasa fulani amehamia chama kingine. Tunahitaji tuwe angalau na vyama vikubwa viwili imara ndani ya nchi kama walivyo Marekani leo kuliko kuwa na utitiri wa vyama usiokuwa na misingi thabiti ya kuiongoza nchi. Demokrasia ndicho kiini cha maendeleo, hivyo vyama vya siasa lazima vijengwe na wenye mioyo ya uzalendo kuliko wasaka fursa.

Mwisho nishauri tu mwanasiasa kuhamahama kunaweza kukusababishia mpaka unazeeka bila kupata unachokitafuta. Ni bora kutulia sehemu moja hata kama kuna dhoruba ya kiwango gani. Dhoruba kwenye siasa ni sehemu ya maisha.

Tabia ya kuhamahama itakufanya usiaminike tena. Wakati unapokewa unaweza kudhani wanakushangilia kumbe unazomewa kwa tamaa na uchu wa kutafuta nafasi kila mahali bila mafanikio.

Siasa ni kama majira ya mwaka. Kuna wakati kunakuwa masika, kiangazi, shibe au njaa, hivyo ni muhimu sana ukishaamua kuwa sehemu tulia. Subra ni muhimu sana vinginevyo utazeeka bila kutimiza malengo.

**0689157789 magabilomjalifu@gmail.com ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Unaikumbuka misemo ya 'dukina', 'dangache'?



Na Adam Fungamwango

**Neno la vijana wa sasa 'tozi' ambalo maana yake ni kijana matanashati, limekarabatiwa tu, lakini linatokana na neno la vijana wa zamani waliloliita 'bitozi'. Maana ni hiyo hiyo moja tu ambalo lilitokana na kundi la muziki wa nchini England, The Beatles ambalo lilivuma na kuwa maarufu sana miaka ya 1960 hadi 1970.**

MAISHA yanakwenda kasi sana. Teknolojia inazidi kupanuka. Kila kitu kinabadilika kadri siku, wiki, miezi na miaka inavyozidi kukatika. Hata maneno na misemo pia vinabadilika.

Maneno na misemo yote, iwe ya kiswahili fasaha na hata ile ya mitaani inakwenda inabadilika kadri ya muda na kizazi kinavyoidizi kubadilika. Ndiyo maana leo neno 'twaa' ambayo maana yake kuchukua hukuti linazungumza na vijana wa sasa, labda tu limebaki kwenye magazeti na hasa kwenye michezo kama vile 'Simba yatwaa ubingwa', Yanga yatwaa Kombe la Mapinduzi', na kadhalika.

Sasa hivi kuna maneno mengine ya kisasa kama vile 'mambo', 'poa', 'unizingua', na mingine mingi ambayo imekuwa maarufu sana, itakuja kipindi nayo itaondoka na kuja misemo mingine pia.

Miaka ya 1970 hadi 1990 kulikuwa na misemo mingine ya rasmi na isiyo rasmi lakini ndiyo ilikuwa inatumika kwa watoto, vijana na hata wazee wa wakati huo. Kwa sasa hata ukiisema kila mtu atakushangaa. Hii inadhihirisha kuwa kuna baadhi ya maneno ya misemo inakuja na kuondoka yenyewe, ingawa iko michache inayobaki.

Leo tutakumbushana maneno na misemo ya zamani ambayo ilikuwa maarufu nchini miaka hiyo, tukianza na 'dukina' na 'dangache'.

Ni msemo maarufu sana miaka ya 1970, ambao ulikuwa hauna maana nyingine zaidi ya salamu hasa kwa vijana kwa vijana au watu marafiki walioshibana. Mmoja akimwona mwenzake humsalimia kwa kusema 'dukina', mwingine ataitikia, 'dangache.'

Hata hivyo, ulikuwa huwezi kuikuta salamu hiyo kwa watu wanaoheshimiana kama baba na kijana wake, mama na binti yake, mtu na mkwewe na wengine wenye nasaba zinazofanana na hizo.

Neno la vijana wa sasa 'tozi' ambalo maana yake ni kijana matanashati, limekarabatiwa tu, lakini linatokana na neno la vijana wa zamani waliloliita 'bitozi'.

Maana ni hiyo hiyo moja tu ambalo lilitokana na kundi la muziki wa nchini England, The Beatles ambalo lilivuma na kuwa maarufu sana miaka ya 1960 hadi 1970.

Lilikuwa kundi la vijana wenye uwezo wa kuimba, kuvaa na utanashati wa hali ya juu, na ilisababisha vijana wengi duniani kuiga uvaaji wao na na hata kuiga aina yao ya kufuga nywele na kujiita 'mabitozi'. Baadaye likaja neno 'chekibobu' ambalo maana yake haikutofautiana na sana na hiyo.

Neno lingine ni 'mama chanja'. Hili lilikuwa na maana ya mama watoto na lilitumiwa sana na wanaume wenye wake zao ambao tayari wameshabarikiwa kupata watoto.

Kuna msamiati ya usemao 'kuzunguka mbuyu'. Maana yake ni rushwa. Rushwa haikuanza leo. Pia zamani yeyote atakayetaka kudai rushwa kwa mwananchi atamwambia 'zunguka mbuyu', ikiwa na maana kuwa atoe rushwa. Na mtoaji atajua anamaanisha nini.

Ukisikia maneno kama 'njagu' au ndata' ujue ni polisi na yalikuwa yakitumiwa sana na wahalifu kutumiana ujumbe ili kuwakwepa.

Kuna neno 'utabana ngenge'. Hili lilikuwa na maana kama vile maneno ya sasa 'utaipata fresh' au kwa kiswahili fasaha 'utakoma'.

Sijajua ilikuwaje hadi likawa na maana hiyo, lakini 'utabana ngenge' linatokana na jina la bendi maarufu wakati huo iliyotua nchini mwishoni mwa miaka ya 1960 kutoka nchini Zaire wakati huo, ikaweka maskani yake nchini hadi mwanzoni mwa miaka 1970 lilipoamua kuhamishia makazi yake nchini Kenya, 'Bana Ngenge.' Ni bendi iliyopendwa mno, ikiwa na wanamuziki machachari wawapo jukwaani na jina lao ndilo lilizaa msamiati huo.

Tukitoa maana ya maneno mengi tutajaza ukurasa mzima, lakini baadhi ya maneno, misemo au misamiati ni kama vile 'gangwe' lililo na maana mbabe, 'kuachwa kwenye mataa', 'tutakula au fitna?' na maneno waliokuwa wakiyasema wanaume wanapojaribu kuwahitaji wanawake,

Ukisikia 'Fatuma' si jina la mwanamke. Lilikuwa na maana nyingine pia. Ni jiwe kubwa ambalo wezi walitumia wakati huo kuvunja nyumba za watu na kuingia ndani kwa nguvu.

Ilikuwa staili moja hivi ya wizi wa kundi. Ni wezi kuanzia wawili hadi 10 au zaidi waliokuwa wakiingia kwa nguvu na kwenye nyumba za watu na kufanya uporaji. Jiwe zito lilillolotumiwa kuvunja mlango ndilo wao waliita 'Fatuma'. Haijulikani hadi leo ni kwa sababu gani.

Lakini hata maofisa wa polisi wanapotoa taarifa zao kwa vyombo vya habari kama umetokea wizi wa aina hiyo, nao husema kuwa wezi wao waliingia kwa kuvunja nyumba wakitumia jiwe kubwa liitwalo 'Fatuma'.

# HADITHI

KWANI mapenzi ni nini? Si kumpenda yule unayemtaka wewe? Kwa nini inafika wakati watu wanapangiana? Je, ukilazimisha yanaitwa mapenzi? Si yatafanana na utumwa? Yeyote anayetaka kulifanya penzi liwe na matabaka, rangi, kabila, anaweza kusababisha maafa makubwa. Donald. Kijana msomi aliyetoka Marekani, anarejea nchini Tanzania. Akakabidhiwa kuendesha kampuni za baba yake lakini pia anatakiwa aoe. Hapo ndipo tatizo linapoanza. Usikose hata nakala moja ya riwaya hii tamu na ya kusisimua.

# Sumu ya Mapenzi-4

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Donald alimvuta msichana huyo akiwa bado ameshika. "Nifuate huku." Alimwambia.

"Na wewe pia njoo." Alimwita mwenzake.

Umati uliokuwa hapo ulikuwa hauelewi nini kimetokea. Burudani yao ya ndondi imekatishwa ghafla na mtu ambaye hawamwelewi vyema. Wengine walidhani kuwa labda ni askari.

Alifungua mlango wa gari na kuingiza mkono, kwenye droo, akatoa kibunda cha pesa na kuhesabu.

"Si umesema laki mbili?"

"Ndiyo."

Alichofanya ni kumkabidhi msichana aliyemshika ili ampe mwenzake aliyekuwa anapigana naye.

"Haya nimekupa hizi, mlipe mwenzako. Ni shilingi laki mbili." Msichana alimpa mwenzake huku akiwa hatazami usoni. Bado Donald alimuweka chini ya himaya yake ili asipigwe. Mwenzake alizipokea.

"Nadhani tayari ameshakulipa, sasa ugomvi uishe. Sitarajii kama mtapigana tena."

"Mimi nilikuwa nataka changu tu, nimeshapata sina shida na mtu." Alisema msichana huyo na taratibu alianza kuondoka na kufuatwa na wasichana mwenzake waliokuwa wanamuunga mkono. Wengine wakishangilia. Donald alibaki amesimama nje ya gari lake pamoja na msichana aliyebaki.

"Pole sana." Alimwambia huku akiwa amemkamata mkono. Alihesabu noti zingine kiasi cha shilingi laki moja.

"Bibie chukua hizi. Umeumia kidogo. Unaona damu zinatoka puani. Nenda kajitibie. Kama hazikutosha basi chukua namba zangu, nipigie kesho nitakuja kulipa."

"Donald imekuwaje tena?" Ilikuwa sauti ngeni iliyosikika. Alipogeuka alipoangalia sura aligundua kuwa ni ya rafiki yake mpenzi, Sadiki. Hata Sadiki kama si maelekezo kuwa atakuja na aina hiyo ya gari asingemfahamu kwa jinsi alivyobadilika.

Walikumbataiana. Ni miaka mingi hawajaonana. Waliongea kidogo, lakini kuna kitu amabcho hakiko sawa.

Donald alimhadithia jinsi alivyofika hapo na mkasa aliuoukuta na jinsi alivyoutatua.

"Tausi? Wewe ndiye ulikuwa unapigana?" Aliitikia kwa kichwa




**"Donald imekuwaje tena?" Ilikuwa sauti ngeni iliyosikika. Alipogeuka alipoangalia sura aligundua kuwa ni ya rafiki yake mpenzi, Sadiki. Hata Sadiki kama si maelekezo kuwa atakuja na aina hiyo ya gari asingemfahamu kwa jinsi alivyobadilika. Walikumbataiana. Ni miaka mingi hawajaonana. Waliongea kidogo, lakini kuna kitu amabcho hakiko sawa.**

"Na nani?"

"Tatu." Ndiyo kwa mara ya kwanza Donald anaisikia sauti ya msichana huyo.

"Donald twende bwana nyumbani, wanawake wa uswahilini utawaweza? Wanaumiza kichwa sana. Kila siku wao kusutana, kupigana. Siku hizi watu wanawaacha tu." Sadiki alimdokeza rafiki yake.

*****************************

Usiku wa siku hiyo ulikuwa wa mateso makubwa. Usingizi haukumjia kirahisi.

Na ulipotaka kumjia tu, basi anasikia kama sauti ya mwanamke inamlilia.

Inamlilia imwokoe. Haikuwa sauti ya mwingine ila ni Tausi. Dada mmoja wa uswahilini Magomeni Makuti. Hakuelewa kwa nini.

Alipoona hapati usingizi, akainuka na kuanza kuzungukazunguka chumbani mwake. Baadaye aliamua kwenda kutafuta japo lepe la usingizi.

Aliamka saa 11:00 alfajiri kitu ambacho si kawaida yake. Ni kwa sababu hakupata usingizi.

Tayari alikuwa ameshaanza kazi kwenye kampuni ya baba yake kama Ofisa Mtendaji Mkuu. Wakati akiingia kwenye gari kwa ajili ya kwenda ofisini alisikia simu yake ya mkononi ikiita.

Alichukua simu yake na kuangalia namba. Haikuwa imeseviwa. "Nani huyu asubuhi yote hii?" Aliwaza.

"Hallo kaka shikamoo." Alikutana na sauti tulivu na msichana ilimwamkia.

Sauti ya mwanamke na kuamkiwa kule kulimfanya ashangae kidogo, lakini hakukumfanya akose kujibu "Marahaba, nani mwenzangu?"

"Samahani kaka, mimi ni yule msichana wa jana kule Magomeni Mapipa. Wewe si yule kama uliyeamulia ugomvi?" Ndipo Donald aliposhtuka na kukumbuka jambo hilo. Alikumbuka kuna kitu kilimfanya asipate usingizi juu ya tukio hilo.

"Okay, nakumbuka, wewe na nani sasa kati ya wale?"

"Mimi ni Tausi, uliyenipa pesa nikajitibie."

Ghafla ni kama moyo wa Donald ulijisikia faraja ghafla.

"Aaa, wewe ni Tausi?" Aliuliza na kusikia kicheko hafifu, lakini kilichomkosha na kukihitaji.

"Ndiyo mimi kaka."

"Enhee unasemaje, mbona asubuhi hivi?"

"Naenda tena hospitali. Jana niliwenda, nikatundikiwa dripu mbili, sindano na vidonge, nikaambiwa leo niende tena. Sasa nilikuwa nimepungukizwa elfu ishirini ili matitabu yakamilike."

Donald ndipo alipokumbuka kuna kitu alimwambia.

"Bibie chukua hizi. Umeumia kidogo. Unaona damu zinatoka puani. Nenda kajitibie. Kama hazikutosha basi chukua namba zangu, nipigie kesho nitakuja kulipa."

Ni ahadi aliyoiweka mwenyewe jana wakati akisuluhisha ugomvi.

"Kwani nini hasa uliumia?"

"Niliumia usoni, mbavu, na kichomi pia kilinipata."

"Pole sana Tausi."

"Ahsante kama yangu."

"Hivi ni kweli ulimkopa na ulikuwa unadaiwa?"

"Ni kweli kaka yangu. Alikuwa ananidai shilingi laki mbili na ilikuwa nilipe, lakini pesa nilizotengemea kwenye mchezo wa upatu niliokuwa tunacheza hazijatoka hadi leo.

Mimi mwenyewe nadai..."

"Basi Tausi, nakutumia shilingi elfu hamsini, elfu thelathini itakuwa ni ya juisi na machungwa. Si unajua mgonjwa lazima ale matunda?" Donald alisikia kicheko kingine kutoka kwa Tausi.

"Nitashukuru sana kaka yangu. Kwani wewe kaka wa wapi, mbona hatujawahi kukuona Magomeni?"

"Usijali Tausi. Mimi si mkazi wa huko. Nilikuja tu kwa rafiki yangu Sadiki, nilisoma naye."

"Ahaa namfahamu si ndiyo yule aliyekuja pale mkaondoka wote?"

"Ndiyo."

"Haya basi ngoja nikate ili nikutumie." Donald alikata simu na kutekeleza alichoahidi.

****************************

"Vipi mbona kama huna furaha na mimi?" "Nimekwambia naumwa wewe nenda kwenu, leo sijisikii vizuri."

"Kama hujisikii vizuri mimi nipo hapa kwa ajili ya kukuliwaza."

"Nimekwambia sitaki kuliwazwa. Mtu analiwazwa akiwa amechoka, siyo kuumwa, unasikia Doris."

"Basi naondoka."

"Nenda."

Zilikuwa sauti za wapenzi wawili. Donald na Doris. Doris alikuwa amepigiwa simu na mama Donald, Eva. Mama ambaye alichangia sana kupatikana kwa Doris, msichana mrembo na msomi ili awe mkwewe. Alimwita baada ya kijana wake kusema kuwa ni mgonjwa.

**ITAENDELEA JUMAPILI**

HABARI BUR



# Country Boy watu wanataka matokeo

CHOCHOTE kinaweza kutokea kati ya rapa kutoka lebo ya Konde Gang, Country Boy na mwanamuziki nyota wa Nigeria, Davido baada ya wawili hao kuonekana wapo pamoja.

Country Boy ameposti picha akiwa na Davido kwenye ukurasa wake wa Instagram na kuandika "Kabla ya maswali ya collabo kwanza mnaweza kutumia hii picha kwa matumizi mengine".

Country Boy na Ibraah ni baadhi ya wasanii kutoka lebo ya Konde Music Worldwide kwa sasa wapo nchini Nigeria katika maandalizi ya Album ya CEO wao mtu mzima Harmonize.



# PNC akikumbuka hili ni majuto

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, PNC ameikumbuka ile ishu ya kumpigia magoti Meneja wake, Ostadh Juma na Musoma, na kusema kitendo kile anakijutia.

Ikumbukwe kuwa kipindi cha nyuma msanii huyo alionekana katika picha akiwa amepiga magoti kumuomba msamaha bosi wake ili kumrudisha katika lebo ya Mtanashati Entertiment.

"Mimi na Ostadh Juma kuna vitu tulipishana na yeye hakupendezwa navyo, halafu mbali na muziki Ostadh alikuwa ananisaidia kama mdogo wake, ile picha ilikuwa ni utani sikuwa 'serious' kama ambavyo watu waliichukulia, nilikuja kuijutia ile picha baada ya maneno ya watu kuwa makubwa". Amesima PNC kupitia kipindi cha Planet Bongo kinachorushwa na East Afrika Radio.



# Tuchel: Sitakasirika nikiwakosa nyota

**LONDON,** England

THOMAS Tuchel ameelezea namna gani anataka kukiimarisha kikosi cha Chelsea wakati wa dirisha la usajili, lakini amesema hatakuwa na "hasira" kama atawakosa nyota anaowawania.

Tuchel alikosana na mkurugenzi wa michezo wa Paris Saint-Germain, Leonardo baada ya kuweka wazi kuwa anahisi mabingwa hao wa Ligue 1 wangeweza kufanya vizuri zaidi kama wangesajili wachezaji zaidi.

Hiyo haikuwa mara ya kwanza kwa kocha huyo raia wa Ujerumani kuweka wazi kile anachokiona kwenye suala la usajili.

Erling Haaland na Romelu Lukaku ni miongoni mwa wachezaji ambao wamekuwa wakihusishwa na mpango wa kuwaniwa pale Stamford Bridge na Tuchel amesema amekuwa akihusishwa kwenye mkipango ya kuimarisha kikosi hicho.


"Nina maoni yangu kuhusu nini tunaweza kuongeza kwenye kundi na kufanya vizuri," alisema Tuchel.

"Hiyo ni kazi yangu. Nitatoa mawazo yangu wakati nitakapoulizwa kuhusu mawazo yangu.

"Tunafanya hivi na wakati mwingine mawazo yako huwa yanabadilika na hiyo pia ni hatua.

"Nina mawazo, bilashaka yoyote. Nina mawazo mengi kuhusu kikosi hiki na aina ya wachezaji ambao ninawahitaji.

"Sio tu jambo la kufikiria kuhusu mchezaji A na B na kama hawatakuja nakuwa na hasira, hapana. Haikuwa kama hivyo kwa kipindi chote cha maisha yangu ya ukocha."





# GUARDIOLA AMTAKA MESSI ASIONDOKE

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola amesema nyota wa klabu ya Barcelona, Lionel Messi hawezi kupata sehemu bora katika maisha yake ya soka kama ilivyo pale Nou Camp.

Hivyo amemtaka nyota huto raia wa Argentina mwenye umri wa miaka 33 kubakia katika kikosi hicho, ambacho amekichezea karibia kipindi chote cha maisha yake ya soka.

Messi mkataba wake wa sasa unamalizika mwishoni mwa msimu huu, na kumekuwa na sintofahamu kuhusu mustakabali wake kwa miamba hao wa Katalunya.

Na sasa kocha wa zamani wa Barcelona, Guardiola amesema kuwa, Messi maisha yake yataendelea kuwa bora zaidi kama akibakia kwa miamba hao.

"Natumaini Lionel Messi anaweza kumalizia maisha yake ya soka Nou Camp, kwa sababu hakuna sehemu nyingine nzuri itakayomfaa zaidi ya hapo katika maisha yake ya soka," amesema Guardiola akinukuliwa na BT Sport.

Guardiola amefikia kutoa kauli hiyo baada ya kuwapo tetesi kuwa klabu ya Paris Saint-German imempa ofa kubwa nyota huyo, ingawa Messi mwenyewe anatarajia kufanya uamuzi wa mustakabali wake mwishoni mwa msimu.

# *Madrid yamwinda Lewandowski*

**MADRID,** Hispania

ROBERT Lewandowski anatajwa kuwa kwenye hesabau za Real Madrid msimu ujao ikiwa ataondoka ndani ya kikosi cha Bayern Munich msimu huu, kwa mujibu wa Sky Sport.

Nyota huyo amekuwa kwenye kiwango bora zaidi cha kucheka na nyavu akiwa amefunga jumla ya mabao 43 katika mechi 37 ambazo amecheza hadi sasa ndani ya Bayern.

Lewandowski mwenye umri wa miaka 32 mkataba wake wa sasa umebakiwa na miaka miwili ndani ya kikosi hicho, ambapo amekuwa akihusishwa kujiunga na Madrid hata kabla ya kujiunga na Bayern akitokea Borussia Dortmund mwaka 2013.

Kwa mujibu wa Sky Sport, Bayern itakuwa tayari kumuuza mshambuliaji huyo kwa dau la euro milioni 52, huku thamani hiyo ikiwa imeshuka kutokana na janga la virusi vya corona.

Wakala wa Lewandowski, Pini Zahavi imeripotiwa kwamba yeye anasikilizia ofa nono kwa ajili ya mchezaji wake na hata ikiwa ni Real Madrid atamruhusu.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# KLOPP AIFIKIRIA LIGI YA EUROPA

### ●●● Asema uwezekano wa kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya ni mgumu, hivyo...

**LIVERPOOL,** England

KOCHA Mkuu wa Liverpool, Jurgen Klopp amesema ataichukulia kwa heshima kubwa michuano ya Ligi ya Europa kama timu yake itashindwa kufuzu kucheza Ligi ya mabingwa Ulaya msimu ujao.

**Mabingwa hao wa Ligi Kuu ya England wa msimu wa 2019-20 kwa sasa wapo nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi, wakipitwa pointi nne na Chelsea waliopo nafasi ya nne, huku zikiwa zimebakia mechi tano ligi hiyo kufikia mwisho.**

Matokeo yake Liverpool inaonekana kwamba, itaishia kufuzu kwenye Ligi ya Europa kwa msimu huu 2020-21 ikiwa ni mara ya kwanza tangu msimu wa 2015-16.

"Tangu nilipokuja England tumecheza mara moja kwenye Ligi ya Europa na tulikwenda fainali mwaka 2016 na Sevilla, ilikuwa faínali nzuri sana," amesema Klopp akiwaambia waandishi wa habari.

"Pia niliwaona Man United wakifurahia kwenye Ligi ya Europa.

"Inategemea upo kwenye mashindano gani na kwa mazingira yapi, lakini mara zote ilionekana kuwa safi.

"Hatutafikiria kwamba, 'Mungu wangu tunatakiwa kucheza hivi'.

"Ni mashindano makubwa na sijawahi kuyawazia, ingawa najua kwamba ni magumu kwa sababu kuna timu bora zinashiriki.

"Naona wazi kwamba, uwezekano wa kufuzu kwneye Ligi ya mabingwa Ulaya msimu ujao ni mgumu, ngoja tufikirie kuhusu nini kitatokea msimu ujao."

Wekundu hao oleo Jumapili watacheza na Manchester United kwenye mchezo wa Ligi Kuu England waliopo nafasi ya pili kwenye msimamo, wakiwa kwenye harakati za kupigania kumaliza kwenye nne bora.

"Kushinda mechi tano hazitatosha, inategemea na namna timu nyingine zitakavyofanya, lakini bila kushinda mechi tano hatuwezi kuwa na nafasi," alisema Klopp.

## ZISIKUPITE

### MESSI KUONGEZA MKATABA

MSHAMBULIAJI wa Argentina, Lionel Messi, 33, atatia saini mkataba mpya Barcelona kwa masharti yaliyopunguzwa. ***(Eurosport)***

### STERLING KUUZWA

KLABU ya Manchester City ipo tayari kumuuza mshambuliaji wa England, Raheem Sterling, 26, msimu huu wa joto. ***(Football Insider)***

### MADRID KUMNASA HAALAND

REAL Madrid inaweza kupata saini ya mshambuliaji wa Borrusia Dortmund, Erling Haaland, 20, kwa mujibu wa wakala wa mshambuliaji huo, Mino Raiola. ***(AS)***

### NEYMAR KURUDISHWA BARCA

BARCELONA imefanya mawasiliano na Paris St-Germain ili wamrudishe, Neymar, 29, pale kwenye uwanja wa Nou Camp. ***(RAC1, via Sport)***

### YAJITOSA KWA RABIOT

CHELSEA wamepania kuikabili Barcelona katika usajili wa Adrien Rabiot, 26, kutoka Juventus msimu huu wa joto, huku kiungo huyo wa Ufaransa akipatikana kwa pauni milioni 17. ***(Calciomercato)***

### ABRAHAM AGOMBEWA

WEST Ham, Aston Villa na Newcastle United ni miongoni mwa klabu zinazovutiwa na mshambuliaji wa Uingereza, Tammy Abraham, 23, huku Chelsea ikiwa tayari kupokea pauni milioni 40. ***(ESPN)***

### TORREIRA KUTORUDI ATLETICO

KIUNGO wa kati wa Uruguay, Lucas Torreira, 25, hatarudi kwa msimu wa pili kwa mkopo kule Atletico Madrid, lakini angependa kujiunga na Boca Juniors. ***(Mundo Deportivo)***

### CASIMIR AFUATILIWA

LEICESTER United, AC Milan na Wolfsburg wanamfuatilia wa nyota wa Le Havre, Josue Casimir, 19. ***(Foot Mercato)***

### O'BRIEN AWANIWA NEWCASTLE

NEWCASTLE United inaweza kufanya harakati za majira ya joto kwa kumsajili wa kiungo wa Huddersfield, Lewis O'Brien, 22. ***(Sun)***

### MCCARTHY AWANIWA

KLABU ya Newcastle inataka kuipiku Celtic kwa kuwania saini ya kiungo wa Crystal Palace na Jamhuri ya Ireland, James McCarthy, 30. ***(Teamtalk)***

### VILLA KUMSAJILI ENGELS

ASTON Villa itamsajili beki mpya wa kat kipindi cha majira ya joto kama sehemu ya kujihami kwa sababu inajiandaa kumtoa beki wa Ubelgiji, Bjorn Engels, 26. ***(Football Insider)***

## Saido ataka kocha Yanga apewe muda

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji wa Yanga, Saido Ntibazonkiza amewataka wanachama na mashabiki wa timu hiyo kumpa muda Kocha Mpya, Nasreddine Nabi ili kukisuka kikosi hicho.

Akizungumza kwenye Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga mara baada ya Yanga kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Prisons kwenye mchezo wa kombe la FA hatua ya 16, alisema kocha huyo amekaa na timu hiyo muda mfupi, na kuna mabadiliko ingawa sio makubwa sana.

"Mabadiliko yapo, ila hawawezi kuwa makubwa sana kwa sasa kwa sababu bado kocha ana muda mfupi. Nadhani tumpe muda timu itakuwa vizuri zaidi," alisema Ntibazonkiza.

Kocha huyo raia wa Tunisia alianza kufundisha timu hiyi karibuni, akichukua nafasi ya Cedric Kaze ambaye alifurushwa ndani ya klabu hiyo baada ya timu kupata matokeo mabovu.

Kuhusu pasi yake ya goli, alisema anashukuru kwa kutengeneza pasi ambayo imesababisha ushindi kwa timu yake na kutinga hatua ya robo fainali.

Yanga ilifanikiwa kuingia hatua ya robo fainali ya Kombe la FA juzi Ijumaa ilipoichapa timu ngumu ya Prisons bao 1-0, lililofungwa na Yacouba Songne mwanzoni mwa kipindi cha pili na kuifanya timu hiyo kuweka rekodi yake msimu iliopita, ilipofanikiwa kuingia hatua hiyo kwa kuichapa Kagera mabao 2-1 Juni 30 mwaka jana.

## Namungo yamaliza CAF bila pointi

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Namungo amemaliza mechi zake za Kombe la Shirikisho Afrika hatua ya makundi, ikiwa haijafunga bao hata moja na pia haina pointi.

Jumatano usiku, Namungo ilihitimisha safari yake ya michuano hiyo kwa kuchapwa bao 1-0 nchini Misri dhidi ya wenyeji wao Pyramids.

Baada ya kipigo hicho, Namungo imemaliza Kundi D ikiwa inashikilia mkia, ikiwa imecheza mechi sita, haijashinda hata mechi moja wala sare, ikifungwa mechi zote sita, ikiwa haijafunga hata bao moja, lakini ikipachikwa mabao tisa.

Alisema kuwa wachezaji wake wengi hawana uzoefu kwenye michuano hiyo, lakini pia timu yake imekutana na timu vigogo na anachofurahi ni kwamba yeye na wachezaji wake kuna vitu wamejifunza.

Namungo ilianza michuano hiyo ya makundi kwa kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Raja Casablanca ya Morocco ugenini, ikachapwa mabao 2-0 nyumbani dhidi ya Pyramids ya Misri, kabla ya kufungwa bao 1-0 nyumbani na ugenini dhidi ya Nkana FC na , ikachapwa mabao 3-0 nyumbani dhidi ya Raja Casablanca, kabla ya kufungwa bao 1-0 Jumatano iliyopita.

# MASHABIKI SIMBA WAWAVAMIA KAIZER

**Na Adam Fungamwango**

KAMA ilivyotegemewa, baadhi ya mashabiki wa Simba wameingia kwenye akaunti ya mtandao wa kijamii wa klabu ya Kaizer Chiefs na kuwashangaza mashabiki wao.

**Mashabiki wengi wa Simba wameingia na kuanza kuwachokoza kwa kuwatania kwa maneno mbalimbali, kiasi kwamba baadhi ya mashabiki wa Kaizer Chiefs kuanza kuulizana kama mashabiki wa timu hiyo wana akaunti ya klabu yao.**

Hii si mara ya kwanza kwa mashabiki wa klabu ya Simba kufanya hivyo, kwani amekuwa 'wakivamia' akaunti rasmi za klabu mbalimbali ambazo wanacheza nazo kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akaunti ya Kaizer Chiefs ilianza kupata wageni mara baada ya kumalizika kwa droo ya Ligi ya Mabingwa Afrika siku ya Ijumaa, ambapo Simba imepangwa kucheza na Wasauzi hao kuanzia Mei 15 hadi 15 kwenye Uwanja wa FNB nchini Afrika Kusini na marudio yake kuwa Mei 21 au 22 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Wakionekana kushitushwa na kutopendezwa na hali hiyo, mashabiki wengi wa Kaizer Chiefs licha ya kuulizana hivyo, lakini waliwataka mashabiki wa Simba kuondoka kwenye ukurasa wao na kwenye kufanya hivyo kwao.

Lakini pia mashabiki walikuwa akimwambia anayesimamia ukurasa huo kuwaondoa mashabiki hao ambao wamekuwa wengi sana na wanaleta fujo kutokana na maneno yao ambao wengi hayaelewi.

Ingawa baadhi mashabiki wa Simba wamekuwa wakiandika kwa lugha ya kiingereza wakiwaambia Wasauzi hao wajiandae kwa kipigo, lakini wengi wamekuwa wakiandika kiswahili na kuwachanganya.

Shabiki mmoja aliuliza wasauzi wenzake kwa lugha ya Kizulu kuwa kila akipitia 'posti' za Watanzania wengi wao wanaandika "Kwa Mkapa Hamtoki", hivyo kuwauliza wenzake lina maana gani. Kwa sasa 'Vita' ya maneno imehamia kwenye ukurasa wa mtandao wa kijamii wa 'Kaizer Chiefs' kati ya mashabiki wa Simba ambao wameonekana kuwatisha mno Wasauzi na kuanza kuwa na wasiwasi.

Mashabiki wa Simba wamekuwa na tabia hiyo tangu kwenye mechi dhidi ya FC Platinum ya Zimbabwe na waliendelea kufanya hivyo kwenye akaunti pia kwa timu za AS Vita ya Congo DR na Al Ahly.



Wachezaji wa timu ya Shule ya Msingi Muhimbili, wakichuana na timu ya Shule ya Msingi Msimbazi Mseto, wakati wa mazoezi ya kujiandaa na mashindano ya Umoja wa Michezo kwa Shule za Msingi katika viwanja vya michezo Jakaya Kikwete, Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Ruvu Shooting yageukia kwenye ligi*

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kusukumizwa nje ya michuano ya Kombe la FA, timu ya Ruvu Shooting imesema kuwa sasa nguvu zao inazielekeza kwenye Ligi Kuu ili kupata nafasi ambayo inaifanya kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa.

Jumamosi iliyopita, Ruvu Shooting ikiwa ugenini, ilichapwa mabao 4-1 kwa mikwaju ya penalti baada ya sare ya bao 1-1 kwa dakika 90 za mchezo.

Msemaji wa klabu hiyo, Masau Mbwire alisema kuwa pamoja na kuondolewa kwenye michuano hiyo, lakini hawakati tamaa, badala yake wanajipanga kwa ajili ya kuendelea na ligi.

"Tumetolewa kwenye michuano ya Kombe la FA, lakini nafasi tunayo kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara kwa sababu bado tuna nafasi ya kuwa kwenye moja kati ya timu nne za juu," alisema Masau.

Huenda Tanzania ikatoa timu nne kwenye michuano ya kimataifa mwakani kutokana na Simba kufika hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, hivyo timu kwenye Ligi Kuu zinapambana kusaka nafasi nne za juu ambazo zinaweza kuwapa uwakilishi.

Tanzania ipo kwenye nafasi nzuri zaidi, kwani timu ya Al Ahly Bengazi ya Libya imekuwa haifanyi vema kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho, hivyo kuipa nafasi Tanzania.

Ikumbukwe kuwa Tanzania na Libya ndizo zinazonyang'anyana nafasi kutokana na kuwa na pointi za chini, ambapo mwaka juzi Tanzania iliiondoa Libya, lakini baadaye nchi hiyo ikachukua nafasi yake na sasa huenda ikanyang'anywa tena.

Kama Tanzania itapata nafasi nne, basi timu tatu za juu zitacheza kimataifa, mbili zikicheza Ligi ya Mabingwa Afrika, na moja Kombe la Shirikisho, huku bingwa wa Kombe la FA naye akienda kwenye Shirikisho.

# Michezo

Jumapili Mei 2, 2021

Nipashe




Klopp aifikiria ligi ya Europa UKURASA 22



Sergio Aguero wa Manchester City (katikati) akifunga bao dhidi ya Crystal Palace wakati wa mchezo wa wa Ligi Kuu ya England baina ya timu hizo, mchezo uliofanyika jana Jumamosi kwenye uwanja wa Selhurst Park. Man City ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

# Gomes: Tuko tayari kwa Kaizer Chiefs

## Asema Simba inataka kufika mbali kwenye michuano hii ingawa...

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba, Didier Gomes amesema kuwa kikosi chake kwa sasa kiko tayari kupambana na timu yoyote kwenye hatua ya robo fainali na wanaisubiria kwa hamu Kaizer Chiefs.

**Gomes amesema hayo mara baada ya kutoka kwa ratiba ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya robo fainali, ambapo wawakilishi wa michuano hiyo nchini, Simba imepangwa kucheza dhidi ya Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini.**

Alisema kuwa Simba inataka kufika mbali kwenye michuano hii na ipo tayari kucheza dhidi ya Wasauzi hao na ingawa haitokuwa rahisi, lakini ana uhakika inaweza kwenda mbali zaidi msimu huu.

"Ni ratiba nzuri. Itakuwa mechi nzuri sana. Kaizer Chiefs ni wazuri na Wekundu wa Msimbazi kwa sasani wazuri sana. Tutacheza mechi ya kwanza ugenini na kumalizia nyumbani. Tutaitumia faida hiyo," alisema Gomes.

Aliongeza; "itakuwa mechi ngumu kwani hatua hii timu zote ni ngumu kwa sababu hata tukipita tutacheza na mshindi kati ya Wydad Casablanca na MC Alger na hakuna timu rahisi kwenye hatua hii tuliyofikia. Lakini msimu huu Simba ni nzuri na inaweza kwenda mbali zaidi.

Kwa upande wake mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya Simba, Haji Manara amesema kwa namna fulani imewapa unafuu kuliko wangepangiwa na timu za Afrika Kaskazini maarufu kama Waarabu.

"Kuna mfanano fulani wa mila zetu kwa timu za Afrika Kusini na sisi kuliko kucheza na timu za Waarabu. Huo ni ukweli ambao haupingiki, ndiyo maana unaona wanachama na mashabiki wa Simba wengi wamefurahi," alisema Manara.

"Hatuwabezi, ila kucheza na timu za kiarabu ni hatari zaidi kuliko hawa wenzetu. Na kwa bahati nzuri tunaanzia ugenini na mechi yetu inayofuata kama tutavuka hapa pia tutaanzia ugenini kwa hiyo itatupa hamasa kubwa.

"Kaizer Chiefs ni timu kubwa, lakini Simba nayo kwa sasa kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati ni timu kubwa pia," alisema.

Simba imepangwa kucheza Mei 14 au 15 mwaka huu kwenye Uwanja wa FNB nchini Afrika Kusini na mechi ya marudiano itakuwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Mei 21 au 22.

# Yanga sasa nguvu zote kwa watani

**Na Saada Akida**

BAADA ya kutinga hatua ya robo fainali ya kombe la Shirikisho, FA, uongozi wa Yanga umesema sasa nguvu zao wanazielekeza kutafuta pointi muhimu kwenye pambano lao lijalo dhidi ya watani wao wa jadi Simba.



Mchezo huo wa pili wa ligi kuu Tanzania bara kuzikutanisha Yanga na Simba mwaka huu, utakaopigwa Mei 8, 2021 kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa.

Kikosi cha Yanga kinachonolewa na kocha, Nesreddine Nabi (pichani) kilipata ushindi wa dhidi ya Prisons katika mchezo wa hatua ya 16 bora ya kombe la FA na kusonga mbele katika hatua inayofuata. Kikosi hicho sasa kinaendelea na maandlizi yao kuelekea pambano lao dhidi ya Simba ambao watakuwa wenyeji wa mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungunza na gazeti hili, Nabi alisema anaendelea kufanyia kazi mapungufu ya kikosi chake kwa ajili ya kujianda na kupata matokeo katika michezo iliyopo mbele yao ikiwemo dhidi ya Simba.

Alisema mikakati yake ni kuona Yanga inaendelea kupata matokeo mazuri katika mechi zilizopo mbele yao ili kuendelea kujiimarisha katika mbio za kuwania ubingwa wa Ligi hiyo.

"Tunaendelea kufanyia kazi mapungufu yetu, kikubwa ni kuhakikisha tunafanya vizuri katika mechi zilizopo mbele yetu, hasa kutafuta pointi tatu katika kila mechi ili kujiweka katika nafasi nzuri kufikia malengo yetu," alisema Nabi.

Alisema ana heshimu Simba ni timu nzuri na ana imani itakuwa mechi ya ushindani mkubwa kwa sababu hata wao wako vizuri na wote wanahitaji pointi muhimu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >